Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Sema: Hakika nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaita kinyume cha Mwenyezi Mungu. Sema: Sitafuata matamanio yenu yasiyokuwa na maana, maana hapo nitapotea na sitakuwa miongoni mwa walioongoka. (*Al An'aam* 6:57).

JUZU 74 No. 179 | RABIUL II/JAMAD I 1435 AH | MARCH 2014 | AMMAN 1393 HS | BEI TSH. 500/=

Mkutano wa dini zote uliondaliwa na Jumuiya:

Watoa matumaini mapya duniani

Na Sheikh Waseem Ahmad Khan - Tabora

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani, Hadhrat Khalifa tul Masih wa Tano ayyadahullahu taala binasrihil aziz (a.t.b.a.) alitoa hotuba ya Ijumaa tarehe saba mwezi wa Machi 2014 katika msikiti wa Baitul Futuh mjini London nchini Uingireza. Katika hotuba yake baada ya kusoma tashahhud na sura Al-faatiha, huzur alisema kuwa takriban wiki tatu zipitazo, jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Uingireza kwa kusherehekea kukamilika kwa karne moja ya Jumuiya nchini humo ilipanga mpango mmoja, ambamo ndani yake masheikh wa dini mbali mbali au wawakilishi wao walialikwa ya kwamba wao kwa kutumia vitabu vyao vitakatifu waeleze mafundisho ya dini zao na nadharia ihusuyo Mwenyezi Mungu na hii pia ya kuwa katika karne ya ishirini na moja kuna kazi na haja gani ya Mwenyezi Mungu? Kwa vyovyote ni dhahiri ya kwamba uwakilishi wa Uislamu ulikuwa lazima upatikane na jumuiya ambao niliuwakilisha mimi, pamoja na hayo kulikuwa na uwakilishi wa Uyahudi, Ukristo, Ubudha, Uhindu, Druzes nk, ambao walieleza mawazo yao na pia kulikuwepo uwakilishi wa Zoroastrianism na Ukalasinga; walikwepo watu wa dini tofauti,vivyo hivyo Bahai vilevile walikwepo. Vile vile baadhi ya wanasiasa na wajumbe wa mashirika ya haki za binadamu pia walipewa nafasi ya kujieleza na mkutano huu ulifanyika katika ukumbi wa hapa uitwao Guildhall ambao ni ukumbi wa zamani wenye historia maalum. Jengo hili ni la 1429 au kutokana na baadhi ya masimulizi lilijengwa hata kabla yake na hii pia inasemekana ya kuwa jengo hili ni moja kati ya majengo mawili ya kale ya London hivyo jengo hili lina umuhimu wake katika historia na kwenye MTA mpango huo umekwishaoneshwa tayari, mtakuwa mmeuona lakini kuhusiana na umuhimu wake wa kihistoria ni matarajio yangu ya kuwa ripoti itakapochapishwa kwenye Alfazl, kumbukumbu yake pia itaelezwa humu.

Kusudio langu la wakati huu si la kuieleza historia yake, kulikuwa na muhtasari wa kitambulisho chake tu, kusudio haswa ndilo hili yakuwa mkutano uliofanywa, niueleze kidogo kuhusu huo. Kama nisemavyo kuwa umekwishaoneshwa kwenye MTA na katika lugha ya Kiurdu pia tafsiri ya hotuba yangu na hotuba za wengine, ni matarajio yangu itakuwa imekwisharushwa tayari lakini kutoka Pakistan nilipata ombi

Endelea uk. 3

Ahmadiyya yatimiza karne moja na robo
Bishara na Shani za Masihi Aliyeahidiwa a.s. zazidi kung'aa

Tarahe 23 Machi 2014, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani, Jumuiya ambayo ilianza katika kijiji kidogo cha Qadiani na sasa imeenea duniani kote imetimiza miaka 125 tangu kuanzishwa kwake kwa amri ya Allah na mtumishi mnyenyekevu wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.

Jumuiya ilianzishwa mwaka 1889 na mwanzilishi Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ambaye alidai ya kwamba ujaji wake umetabiriwa katika hadithi ndani ya vitabu vya Waislamu, lakini pia katika vitabu vya Wakirsto, Wayahudi na dini zingine pia. Alijizatiti katika kueneza ujumbe wa msingi wa Islam ambao ni amani na uvumilivu ili kuepukana na vita ukandamizaji na uonevu.
Akieleza sababu ya kudhihiri kwake Hazarat Mirza Ghulam Ahmad a.s. anasema:



Masjid Fazal Tabora - Msikiti wa kwanza wa Ahmadiyya kujengwa nchini

Nia yangu, dhamira yangu na makusudio yangu ni kuwatumikia binaadamu. Ni wajibu wangu, wajibu wa imani yangu, jazba yangu na njia yangu ya maisha kutumiza hayo.

Jumuiya hivi leo imeunganika chini ya Khalifa wa Tano Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. ambaye anaishi London Uingereza. Chini ya uongozi wake Jumuiya hii imejitokeza kuwa mtetezi wa wanyonge kwa kutoa huduma za kijamii katika nchi zinazoendelea na kupaza sauti ya amani na suluhu kwa mataifa yote na dini zote.
Hazrat Mirza Masroor Ahmad anasema:
Jumuiya ya Ahmadiyya ni Jumuiya ya amani ambayo inatekeleza mambo yake yote kwa kufuata mafundisho ya dini ya Islam. Ni amani pekee inayotawala katika kila tendo letu.

Kuikumbuka siku hii ya kihistoria, Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. alitoa ujumbe maalum kwa watu wote bali hasa kwa Waarabu kupitia kituo cha matangazo cha kimataifa cha Jumuiya – Muslim Television Ahmadiyya – MTA.

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KARNE MOJA NA ROBO ILIYOPITA USHAHIDIWA UKWELI WA AHMADIYYA

Karne moja na robo iliyopita kwa amri ya Allah mtumishi mnyenyekevu wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s, alipewa amri ya kupanda mti, mti ambao matunda yake yatamrejesha mwanadamu kwa Mola wake, matunda yatakayodhihirisha shani na utukufu wa Mtume Muhammad s.a.w, ubora wa Qurani Tukufu ukilinganishwa na vitabu vingine.

Kilikuwa ni kicheko na kebehi na wengi walitabiri ya kuwa mti huo utasinyaa, utanywea na hatimae kukauka. Na utabaki hauna kazi yoyote ile isipokuwa kuwa kuni kwa wale wanaotaka kupika dengu na chapati.

Hata hivyo, wenye jicho la yakini, jicho linaloweza kuingia katika mbegu ya wakati na kuweza kujua mbegu inayoweza kuota na ile ambayo haiwezi kuota hawakuwa tayari kuangua kicheko na kufanya masikhara. Jicho hilo liliwapeleka mbali na katika umbali huo wakaona wapandaji wa miti waliopita wakifanyiwa kebehi na kuchezewa shere walimuona Mpandaji aliyepanda mti akichekwa na wote wakati anajenga safina na wao walicheka mno kwa sababau hawakuona dalili yoyote ya hata tone moja la mvua kudondoka lakini aliendelea na kuweka pamba masikioni mwake. Nabii Saleh alichekwa na watu na kumkebehi na kufikia hatua ya ngamia wake kukatwa miguu. Shuaib hakusalimika. Musa alihangaishwa mno hadi wafuasi wake wakafanya ndama sehemu ya ibada. Nabii Yusuf alitumbukizwa katika kisima na ndugu zake wakashangilia na kusema huo ulikuwa mwisho wake. Nabii Ibrahimu a.s. walimtupa motoni lakini moto ukawa baridi kwa Ibrahim. Nabii Issa a.s. walimweka masalabani hakufia pale hivyo shabaha yao haikutimia.

Hivyo wenye jicho la yakini wakajiunga na mpedwa huyu wa Mwenyezi Mungu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., na wakaanza kumwagilia mti huo. Wakati wote huo mashaka yalikuwa mengi, *upinzani mkali, jua la kuchoma hadi unyayoni na kutoka juu ikasikika sauti ikitangaza ni Mimi na Mitume wangu ndio tutashinda na wakazidishiwa imani walipoambiwa je Mwenyezi Mungu hatoshi kwa mtumishi wake?*

Mti huo wa neema za Allah umekuwa na unazidi kustawi. Matunda yake kochokocho na walio pembeni mate yanawadondoka. Mti huo matawi yake yameenea duniani kote na yanafanya kazi kubwa katika nchi 204. Masingizio dhidi ya Mtukufu Mtume s.a.w. yamefukiwa. Qurani tukufu imetafsiriwa katika lugha 71. Vitabu lukuki juu ya mada mbalimbali vimechapishwa wafuasi wa mpandaji huyu wamegeuza ramani ya dunia, tunamzungumzia Sir Muhammad Zafrullah Khan na Profesa Abdul Salaam.

Kwa ujumla hatuna budi kuanguka kwenye kizingiti cha Allah na kutoa shukurani kwa kuulinda mti huu. Na hatimae kula matunda yake. Kwa karne moja na robo kazi nzuri imefanyika kwani ukweli ni kwamba mti hujulikana kwa matunda yake. Lakini safari yetu bado na katika maneno ya Robert Frost ambaye Khalifa Mtukufu wa Nne Hadhrat Mirza Tahir Ahmad r.h. alipenda sana kumnukuu: "*Tuna maili nyingi za kutembea kabla hatujapumzika*" ndio ukweli ambao anausisitiza sana Khalifa Mtukufu wa Tano Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a.

Khalifa mtukufu wa Tano anaeleza ya kwamba sehemu ya pili ya safari yetu ni lazima sote tujitahidi kusafisha nafsi. Mtukufu Mtume s.a.w. anapoambiwa kuwa hakika mnao mfano mwema na sisi sawa na uwezo wetu na nafasi zetu tuwe mfano kwa waliotunzunguka. Tutambue kuwa sisi hatumuoni Mwenyezi Mungu bali yeye Anatuona na tuwapo wawili wa tatu ni Mwenyezi Mungu. Na Quran tukufu inasisitiza ya kwamba amri zote 700 zilizomo katika kitabu hicho kitukufu zinatakiwa zifuatwe katika maisha yetu ya kila siku. Hakuna sheria iliyo ndogo. alichokikataza Allah tukiache na alichotuhimiza tukitekeleze.

Mafanikio hayaji isipokuw kwa kumtegemea Allah, tuna wajibu basi wa kumkabidhi Allah mali zetu, maisha yetu, nafsi zetu, kifo chetu na huu hasa ndio ufaulu mkuu na shabaha ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

Malfudhaat Sayedna Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Mcha Mungu hupata riziki ya kiroho.

Seyydna Ahmad as anasema ya kwamba Mwenyezi Mungu Humruzuku mchaMungu kwa kupitia mpango maalum, hapo nitaeleza riziki ihusuyo maarifa. Mtukufu mtume wetu saw licha ya kuwa (ummi)yaani asiyejua kusoma, alikuwa na kazi ya kupambana na watu wa ulimwengu wote wakiwemo watu wa Kitabu, wanafalsafa, wataalamu wa hali ya juu na maulamaa nk. Lakini alipata riziki ya kiroho kiasi hiki kwamba aliwashinda wote na kutoa makosa yao. Hii ilikuwa riziki ya kiroho isiyokuwa na mfano. Kwa kubaini shani ya mchaMungu, imeandikwa katika sehemu nyingine ya kuwa, Si marafiki zake isipokuwa wachaMungu tu. AL-ANFAAL 35, yaani mawalii wa Mwenyezi Mungu ni wale ambao ni wachaMungu, basi neema hii ni ya namna gani kwamba kwa kupata shida kidogo tu, mja Wake aitwe mpendwa wa Mungu. Katika zama hii za leo ikiwa hakimu au afisa yeyote amwambie mtu fulani ya kwamba, wewe ni rafiki yangu au ampatie kiti au kumheshimu, basi mtu huyo anajivuna na kujifaharisha, lakini mtu huyu atakuwa na cheo kikubwa kiasi gani ambaye Mwenyezi Mungu Amwite na kumtaja kuwa walii na rafiki Yake? Mwenyezi Mungu Aliahidi kwa kupitia kauli ya Mtukufu Mtume Muhammad saw kama ielezwavyo katika hadithi moja ya Kitabu cha Bukhari, Imesimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah r.a.ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Hakika Mwenyezi Mungu Alisema: Yule aliye adui wa rafiki yangu namtangazia vita. Mtumishi wangu hawezi kunikurubia kwa kitu ninachopenda sana kuliko yale niliyomfaradhisha. Na mtumishi wangu hunisogelea kwa njia ya nafali mpaka naanza kumpenda. Na nimpendapo ninakuwa masikio yake ambayo anasikia kwayo,na macho yake ambayo anaona kwayo,na mkono wake ambao anashika kwao, na mguu wake ambao anatembea kwao. Na aniombapo nampa, na atakapo ulinzi wangu namlinda (Bukhari)yaani Mwenyezi Mungu Anasema kwamba walii wangu hupata mapenzi yangu ya aina hii kwa kupitia sala ya nafali.

FARADHI NA NAWAFALI.

Mema anayofanya binadamu yanakuwa na sehemu mbili yaani faradhi na nawafali. Faradhi ni jambo linalomlazimu mtu kulitimiza kama vile kulipa deni au badala ya wema kutenda wema, sanjari na faradhi hizi zote kunakuwa na nafali kwa kila kitendo chema, yaani wema ambao uwe wa ziada baada ya kutimiza haki yake, hizi ni nafali. katika hadithi hiyo imebainishwa kuwa wajibu wa mawalii waendelea kukamilika kwa kupitia nafali, kwa mfano pamoja na kutoa zaka , wanatoa sadaka nyingine. Mwenyezi Mungu Huwa Rafiki ya watu hao. Mwenyezi Mungu Anasema ya kwamba Urafiki Wake wafikia hatua hii ya kuwa Yeye Anakuwa mkono,miguu mpaka ulimi wake ambao anaongea kwao.

KILA KITENDO KIENDANE NA RADHI YA ALLAH.

Jambo ndilo hili ya kuwa binadamu kwa kujitakasa nafsi yake na kuepukana na ubinafsi anatembea chini ya matakwa ya Mwenyezi Mungu basi kitedno chake chochote hakiendi kinyume cha matakwa ya Allah bali kila kitu afanyacho kinakuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Pale ambapo watu wanashikwa na mitihani basi sababu yake inakuwa matendo yao ambayo yanakuwa kinyume cha radhi ya Allah.Radhi ya Allah inakuwa kinyume chake na mtu huyo anashikwa na tamaa zake za nafsi, kwa mfano kwa kupatwa na hasira anafanya kazi ambayo inasababisha kesi zipatikane dhidi yake, lakini kama mtu awe ana nia ya kuwa hatafanya tendo lolote kinyume cha matakwa ya kitabu cha Mwenyezi Mungu na katika kila shughuli yake atakirejea Kitabu cha Mungu, basi ni jambo lililohakikishwa ya kuwa Kitabu cha Mungu lazima kitamshauri kama Alivyosema; wala kilichorutubika, wala kilichoyabisika, ila yamo katika kitabu kidhihirishacho. Al-Anaam 60.

Basi kama sisi tunuie ya kuwa tutachukua ushauri kutoka kitabu cha Mungu,basi ni lazima tutapata shauri, lakini anayefuata matamanio ya nafsi yake lazima atapata hasara na kutiwa kwenye mtihani, kinyume cha hayo Mwenyezi Mungu Alisema ya kuwa mawalii yaani marafiki zangu wanaoongea nami na kufanya kazi chini ya matakwa yangu ni watu ambao wamekwishajitupa mbele Yangu. Kwa kuwahami Mwenyezi Mungu Anasema kwamba ,yule aliye adui wa rafiki yangu namtangazia vita. yaani anayepambana na rafiki yangu hupambana nami, sasa angalieni ya kuwa shani ya mchaMungu iko juu kiasi gani? na cheo chake ni kikubwa kiasi gani mbele ya Allah ya kuwa ana mapenzi ya Mungu ya aina hii ya kwamba kukerwa kwake ni kama kukerwa kwa Mungu, basi kwa kiasi gani Mwenyezi Mungu Atakuwa msaidizi wake.

ANAYEMJIA MCHAMUNGU NAYE PIA HUOKOLEWA.

Seyydna Ahmad as anasema,watu wanashikwa na mabalaa mengi lakini wachaMungu huokolewa nayo bali anayewaendea naye pia anasalimishwa. Masaibu yanakuwa hayana kikomo, mwili wa binadamu umejawa na matatizo mengi ambayo hayawezi kukisiwa, angalieni magonjwa tu ambayo yanatosha kwa ajili ya kumletea matatizo mengi kwa binadamu, lakini anayeishi katika ngome ya Taqwa anaepukana nayo na yule ambaye yupo nje ya ngome hiyo basi yumo katika msitu ambao umejaa wanyama washambuliaji.

MCHAMUNGU HUPATA HABARI NJEMA KATIKA DUNIA HII.

Kuna ahadi nyingine kwa ajili ya mchaMungu yaani wao wanazo habari njema katika maisha ya dunia na katika akhera (Yuunus 65) yaani wachaMungu hupata habari njema katika dunia hii hii kwa kupitia ndoto za kweli bali zaidi ya hayo wanakuwa wenye kupata ruya nao wanapata bahati ya kuongea na Mungu. Wao katika libasi ya ubinadamu huona malaika kama Alivyosema kuwa, Hakika wale wanaosema, Mola wetu ni Mwenyezi Mungu, kisha wakaendelea kwa kudumu, huwateremkia Malaika (Haa Miim 31) yaani wakati wa majaribio mtu huyo anaonesha ya kuwa,yale ambayo niliyoyaahidi kwa mdomo wangu sasa nayatimiza kwa matendo yangu.

Mwenyezi Mungu Atujaalie kutekeleza hayo yote na tuweze kuwa wachaMungu wa hali ya juu ambao kwa sikuzote Mwenyezi Mungu Huwapenda na kuwasaidia kutoka kwake. Aamin.

(Malfudhaat Jalada la kwanza kurasa 9,10)

Mfasiri, ***Sheikh Waseem Ahmad Khan*** - Tabora

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Mkutano wa dini zote uliondaliwa na Jumuiya

Kutoka uk. 1

moja la kuwa itakuwa vizuri kama nieleze mambo yaliyojiri katika mkutano huu mkubwa katika hotuba yangu kama ninavyoeleza kuhusu ziara zangu ili wasikilizaji waweze kuelewa vizuri zaidi na kufahamu umuhimu wake na kujinufaisha nayo pia.

Baadhi ya vipindi vya MTA baadhi ya watu hawavioni, hapa pia jana nilikuwa nikiangalia barua moja isemayo kuwa mimi nilisoma katika gazeti fulani habari ya mkutano huu ijapokuwa ilikuwa ikirushwa kwenye MTA hivyo ni vizuri kwani hotuba watu wanazisikiliza zaidi hivyo nitaeleza muhtasari wake lakini itakuwa bora zaidi ya kuwa ikirushwa kwenye MTA, wanajumuiya wanapaswa kuitazama, hafla ilikuwa nzuri sana.

Wakati huu nitaeleza muhtasari wa hotuba zilizotolewa na wazungumzaji na muhtasari wa yale niliyoyaeleza mimi na pia nitaweka mbele yenu maoni ya wageni mbalimbali ili mambo ambayo yanaonesha msaada na fadhila za Mwenyezi Mungu yawe yanadhihirika na ili dunia itambue ubora wa Islam, ubora wa Mtume saw, ambao umedhihirishwa na ashiki wake mkweli duniani, uwe wazi kwa watu wa dunia na juu yetu. Kuhusiana na mkutano huu jambo la kwanza nitakalosema kabla sijaeleza maelezo mengine ndilo hili ya kuwa wasimamizi wa Jumuiya ya Uingireza ambao walifanya mkutano huu muhimu na mkubwa, hawakutangaza kuhusu mkutano huu jinsi walivyopaswa kuutangaza yaani kabla ya mkutano na waliridhia juu ya hilo tu kwamba wanafanya mkutano na kiasi hiki watu watakuja japokuwa huu ulikuwa muda wa kueneza utambulisho wa jumuiya na kuwaambia watu kuhusu mafundisho mazuri ya Islam. Kama wangekuwa na mawasiliano mazuri na vyombo vya habari basi kazi ambayo inaendelea kufanywa na Amir sahib na timu yake sasa, wanatoa habari kwenye magazeti au zenyewe zinapigwa chapa na zinawekwa vizuri zaidi humo, siku hizi vyombo vya habari ni njia moja kubwa sana ya kufikisha ujumbe na kuhusiana na hilo katika jumuiya nyingi za dunia jinsi ilivyotakiwa kufanywa kazi hiyo haifanyiki na uvivu unaoneshwa sasa huku Marekani wamejitahidi katika hilo, kwa fadhila ya Allah wanafanya kazi nzuri, katika bara la Afrika katika nchi za Ghana na Seraleon kazi inaendelea kufanywa vizuri na sasa katika baadhi ya nchi zingine za Afrika yaani nchi zinazoongea Kifaransa pia zimeelekea upande huu.

Kwa vyovyote tunapaswa kuwa na mawasiliano na vyombo vya habari katika ngazi zote ili kwa kupitia mawasiliano hayo fundisho la Uislam lijulikane kwa dunia na katika mahubiri kasi ipatikane kwani hii pia ni njia moja kubwa ya kufanya mahubiri, jumuiya zinapaswa kuelekea upande huu.



Sehemu ya wasikilizaji kwenye mkutano wa dini zote uliofanyika kwenye ukumbi wa Guldhall Uingereza tarehe 11 February 2014

Sasa naeleza muhtasari wa yale yaliyojiri humo. Baadhi ya wazungumzaji walizungumza mambo mazuri sana. Mwenyezi Mungu Awajaalie kutenda sawa na kile walichokisema na kiwe sauti ya moyo wao.

Mtu wa kwanza ni Bwana Mahesh Chandar Sharma ambaye ni mwenyekiti wa baraza la Kihindu hapa, yeye anasema ya kwamba mada ya leo ina mvuto mkubwa, inathibitika ya kuwa sisi sote tumeafikiana ya kuwa katika ulimwengu huu dhati ya Mungu Ipo. jambo la pili ambalo ni wazi sana ndilo hili kwamba wanasiasa na nidhamu zingine zimeshindwa kustawisha amani duniani, pande zote ugomvi na ufisadi vimeenea kote na watu wamekosa imani juu ya wanasiasa hivyo kwa mtazamo wangu mimi muda umewadia ya kuwa sisi kwa ajili ya kuutakia ubinadamu heri tuelekee tena upande wa dini, sisi tutapaswa kujizoesha sawa na mafundisho ya dini zetu kisha anasema huyu ya kwamba jambo lililo muhimu zaidi ndilo hili ya kuwa sisi tusiendelee kuwanasihi watu wetu tu bali tuwe tunawaonesha mifano yetu pia. Na huu ndio uhakika, Mwenyezi Mungu Amjaalie mzungumzaji huyo pia aweze kutenda sawa na yale ambayo aliyasema.

Kisha ujumbe wa Dalai Lama, kiongozi wa Ubudha ulisomwa na mwakilishi wake naye alisema ya kwamba dini zote zinawafundisha wafuasi wao somo la mapenzi, uungwana na uvumilivu kati yao, hivyo hata kama itikadi zao ziwe zinatofautiana kwa kiasi gani na itikadi zetu, twapaswa kuwaheshimu. Kila dini kweli imeupa ubinadamu mafundisho ya hali ya juu katika wakati wake na katika siku za usoni mafundisho hayo hayo ya kidini yatatufaa katika kuleta duniani amani, upatanifu na maelewano na kutuongoza kwa ajili ya kuishi kwa pamoja. Twapaswa kuiga khulka zile za juu katika maisha yetu ya kila siku ambazo dini zetu zinatufundisha; kwa vyovyote mazungumzo yake haya ni mazuri sana. Anasema yakuwa ufisadi kwa jina la dini unatokea wakati ambapo sisi hatuelewi shabaha na kusudio haswa la dini, anasema kwa muda fulani nilikuwa nikifikiri ya kwamba sisi tunatakiwa kuandaa mipango kwa pamoja ambayo iweze kuwajumuisha wana dini wa kimataifa ili hali ya makubaliano na maelewano ipatikane baina yetu na amani iweze kustawi duniani, anasema kwamba mimi naipongeza Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kwa kuichukua hatua kubwa sana yenye ujasiri ya kuandaa mkutano wa dini wa kimataifa tarehe 11 February 2014 nchini Uingireza, nina imani ya kuwa mikutano ya aina hiyo inakuwa sababu ya kuleta mabadiliko mengi katika mustakbali, kwa vyovyote wazungumzaji wengi wamesema yale ambayo yanahitajika katika zama za leo.

Kisha kiongozi wa kiroho wa dhehebu la Druzes Sheikh Mwafak Tarif anasema, sisi ni taifa ambalo lina mahusiano na dini zote zilizopo katika ardhi takatifu, dhehebu hili linapatikana zaidi katika maeneo ya Israeli na Palestina pia lipo katika Syria. Anasema ya kuwa ardhi takatifu ni ardhi ile ambapo dini nyingi zilipatikana na safari ya kiroho ya mitume wengi ilianza humo, anasema ya kuwa katika Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Anasema ya kuwa, Enyi watu kwa hakika Tumewaumbeni katika kiume na kike, na Tumewafanyeni mataifa na makabila ili mjuane; hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Allah ni Mjuzi, Mwenye habari. Hii ni sura Al-Hujuraat aya ya 14 ambayo alisoma yeye na anasema ya kwamba mimi namshukuru Imamu wa Jumuiya ya Ahmadiyya kwamba yeye na jumuiya yake wamenialika katika mkutano huu nami ninaipongeza Jumuiya kwa kuandaa mkutano huu adhimu kwa kusherehekea kukamilika kwa miaka mia moja hapa Uingireza. Dhehebu letu la Druzes lina mahusiano mazuri na Jumuiya katika Ardhi Takatifu, sisi tumefurahi sana kwa kuupokea mwaliko huu kutoka kwenu, njooni tukiwa pamoja tukemee dhuluma na uchokozi na kuzipanda zile mbegu za mapenzi ambazo ziwe sababu ya kububujika kwa chemchem za mapenzi, si katika mashiriki tu bali katika ulimwengu wote.

Kisha askofu mkuu wa Kanisa Katoliki Kevin McDonald alisema, nimefurahi sana kwa kushiriki katika mkutano wa dini wa kimataifa na kutoa hotuba humo, wakati huu dunia inahitaji sana mikutano ya aina hii. Kisha baadaye alisoma ujumbe wa Kardinal Peter Turkson ambaye ni mwenyekiti wa baraza la Papa na pia ni mshauri wa uadilifu na amani: Ya kwamba mimi nimefurahi sana kwa kutoa hotuba mbele yenu katika mkutano ulioandaliwa na Jumuiya kwa kusherehekea karne moja ya Jumuiya ya Ahmadiyya hapa Uingireza. Jambo lililo muhimu sana la mkutano huu ni hili ya kuwa wajumbe wa dini mbalimbali wa kimataifa kwa kukusanyika hapa wanazungumza kuhusu amani ya dunia.

Bwana Rabbi Professor Daniel Sperber aliyewakilisha Chifu Rabbi wa Israeli alisema kuwa tunaishi katika mazingiria ambapo maendeleo ya dunia yanafahamika kuwa ufaulu mkubwa sana na tofauti ya kiuchumi kati ya maskini na matajiri inaendelea kuongezeka sana. Kwa jina la maendeleo tunatumia neema za dunia kwa kiasi cha kuzipoteza, tunachafua maji safi na kuharibu mapori, sisi tunaishi katika mazingira ambapo kuna mzozo wa dini na siasa pande zote na ufisadi upo. Jina la Mwenyezi Mungu na muongozo Wake Aliotoa unadhalilishwa na hayo yote yanafanywa kwa kutumia jina la busara, maelewano na mahitaji ya kisiasa; njooni tukiwa pamoja tufanye kazi dhidi yake. Mwenyezi Mungu Awajaalie viongozi wao vilevile kuyaelewa hayo na hao waweze kuwaambia pia.

Kulikuwa na baadhi ya ujumbe kutoka wanasiasa na hotuba zao.U jumbe wa Rais wa Ghana uliosomwa na balozi wake, ingawa mwakilishi wake pia alikwepo huko. Yeye aliandika ya kuwa wakati huu kwa mara nyingine tumeambiwa ya kuwa Mwenyezi Mungu Aliwatuma mitume Wake wapendwa duniani ambao walitoa ujumbe huu kwa watu wa dunia bila kuwatofautisha kwa msingi wa rangi na ukoo ya kuwa binadamu anapaswa kuishi maisha yake kwa kutumia njia za amani, utaratibu na uungwana. Kisha aliandika kuhusu halmashauri ya amani iliyoundwa huko Ghana, ambapo kuna mwafaka wa dini na uwakilishi wa dini zote upo. Kisha kuna mwanasiasa wa hapa Baroness Saida Warsi pia alikwepo, naye anasema ya kuwa kuzungumza mbele ya wageni waheshimiwa ni heshima kwangu, mkutano huu unathibitisha kwamba Jumuiya Ahmadiyya ina moyo mkubwa na ina khulka njema ya kwamba mmepanga sherehe ambamo badala ya kuzungumza kuhusu itikadi za Jumuiya yenu, mmewaalika viongozi wa dini mbalimbali ili nao pia watoe maoni yao. Msaada unaotolewa na Jumuiya kwa faida ya binadamu, athari na matokeo yake yanaonekana wazi wazi na kwa sababu ya mkutano huu hii pia imethibitika kwamba viongozi wa dini mbalimbali wako tayari kwa kupatana na kuelewana nami naona ni heshima kwangu kushiriki katika mkutano huu.

Kisha kuna Bi Daktari Qatrina ambaye ni makamu mwenyekiti wa tume ya kimataifa ya kutetea uhuru wa dini huko Marekani na ni rafiki wa Jumuiya tangu siku nyingi; anasema ya kwamba bahati hii aliyoipata ya kufika hapa na kushiriki mkutano huu, mimi nimefurahi sana. Sherehe hii iliyopangwa kwa kukamilika karne moja ya Jumuiya ya Uingireza

Endelea uk. 4

Mkutano wa dini zote uliondaliwa na Jumuiya

Kutoka uk. 3

imenifurahisha sana. Anasema sherehe hii imepangwa kwa ajili ya kutambulisha udugu na uhuru wa dini na huu ndio msingi wa Jumuiya Ahmadiyya. A nasema kwamba Jumuiya Ahmadiyya ni mfano mzuri wa jambo hili kwamba amani ya dini inapatikana katika udugu kwa sababu ya kuwa na uhuru katika dini. Tunapoangalia karne iliyopita, tunakuta kwamba mfano mzuri unapatikana katika karne ile. Katika karne ile watu walipatikana waliofanya juhudi ya kuleta amani duniani kisha alitoa mifano kadhaa ya watu mbalimbali na aliendelea kusema kwamba katika karne ya ishirini tunaona jumuiya yenu kwa namna gani ilizungumza kuhusu dhuluma iliyotendeka duniani. Huzur anasema hapo amekosea, kwa hakika tangu aje Syedna Ahmad a.s, Jumuiya iliendelea kuongea dhidi ya dhuluma na yote ifanywayo ni sawa ya mafundisho ya Syedna Ahmad a.s. Huzur anasema huyo badala ya kusema karne ya ishirini angetakiwa kusema karne ya kumi na tisa. Anasema tunaona katika karne ya ishirini jumuiya yenu jinsi inavyozungumza dhidi ya dhuluma iliyotendeka duniani, nyinyi mmeshika bendera ya uadilifu duniani, mnataka amani katika jamii ambapo watu wa dini mbalimbali waishi kwa amani, waweze kusikilizana na sisi hatuwezi kusikilizana mpaka tuwe na heshima kwa ajili ya wote na tuheshimiane. Naheshimu jambo hili kwamba jumuiya inatoa somo la udugu na kila mmoja wetu awe huru katika kufuata dini na vilevile tunapobadilishana mawazo, tubadilishane mawazo kwa uadilifu. Nina hamu ya kwamba kwa ajili ya lengo hili sisi sote tuweze kufanya juhudi pamoja. Huzur anasema Mwenyezi Mungu Ajaalie viongozi wa nchi zenye nguvu pia kuelewa jambo hili.

Ujumbe wa Waziri Mkuu wa Uingireza pia ulisomwa na Mwanasheria Mkuu Mstaafu wa hapa Bwana Damne Grieve lakini kabla ya kusoma ujumbe wa Waziri Mkuu alitoa maoni yake pia. Alisema kabla ya kusoma ujumbe nataka kusema kwamba sehemu iliyochaguliwa kwa ajili ya mkutano ni nzuri sana, kwa sababu hii ndiyo ni sehemu ambapo wazungu mwanzoni walianza kusaidia dunia nzima na leo kujumuika kwetu hapa ni matunda yake. Mkutano huu ni mkutano wa aina yake, mimi kwa kuwa mkristo nina uzoefu kwamba mtu aliyefuata dini yoyote anaelewa maoni na fikra za watu wengine vizuri kuliko ambaye hafuati dini yoyote. Huzur anasema Mwenyezi Mungu Amjaalie kuelewa jambo hilo vizuri kisha baadaye alisoma ujumbe wa waziri mkuu kwamba mimi naipongeza jumuiya Ahmadiyya kwa sababu ya kuwajumuisha viongozi wa dini mbalimbali katika sehemu moja. Mimi naheshimu sana msaada mkubwa wa Jumuiya Ahmadiyya katika Uingireza.Ikiwa upande mmoja mnafanya mkutano wa dini mbalimbali upande mwingine katika mafuriko yaliyotokea hivi karibuni mmewasaidia watu.Huzur anasema kwamba Khuddam ul Ahmadiyya ilifanya kazi nzuri sana katika mafuriko hayo yaliyotokea hivi karibuni. Anasema kuhusiana na suali la kuelewana mkutano wa leo unashuhudia kwamba nyinyi mko makini kiasi gani katika kazi hii,Mwenyezi Mungu Ajaalie watu wote wajumuike kwa pamoja na amani ipatikane duniani na nimefurahi kwamba mwakilishi wa serekali ya Uingireza pia ameshiriki katika mkutano huu.Sisi kwa kukaa na kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya na viongozi wengine tutatafakari kuhusu hii ya kwamba dini mbalimbali kwa kusaidiana namna gani zinaweza kuleta amani duniani. Kisha ujumbe wa Malkia pia ulisomwa ambaye ni Mkuu wa kanisa la Anglikana,katibu wa Malkia aliandika kwamba mkutano uliopangwa kwa kusherehekea miaka mia moja ya Jumuiya ya Uingireza katika Guildhall,ninafurahi kwa kutuma ujumbe wangu,Malkia alifurahi sana kwa kujua malengo ya mkutano huu na anashukuru kwa kupata mwaliko,anafanya maombi kwamba mkutano huu ufanikiwe kwa njia zote.

Huzur anasema haya yalikuwa maoni ya viongozi mbalimbali. Sasa niliyosema kule naona nieleze muhtasari wake kwa sababu inaonekana watu wengi hawakusikiliza hotuba yangu na haikutolewa vizuri kwenye magazeti pia.Nilisema hii ya kwamba Mwenyezi Mungu Anataka kurekebisha hali ya binadamu na ili watu waweze kutimiza haki za Mwenyezi Mungu na viumbe vyake.Na kwa ajili ya lengo hili Mwenyezi Mungu Anatuma manabii wake duniani.Wale wanaowafuata manabii hufaulu na wanaokataa manabii wa Mwenyezi Mungu huangamizwa.Mataifa yaliyopinga manabii na wale waliokataa Mungu na kusema kuwa hakuna Mungu wala adhabu yake,mataifa ya aina hii yote yaliangamizwa na historia yaoimeelezwanaKuraniTukufu vilevile vitabu vya dini zingine vinaeleza historia ya watu wa aina hii kwamba waliokataa manabii wa mwenyezi Mungu waliangamizwa wote,hivyo tuwe tunafikiria ya kuwa mambo haya si visa bali historia ya kila dini inathibitisha ya kuwa mambo hayo yalikuwa kweli na nilisema kwamba kitabu ninachokiamini ni Kurani tukufu na kitabu hiki kinatuambia kwamba Mwenyezi Mungu kwa kutuma manabii wake Anataka kuthibitisha kwamba mwanadamu kwa kupata imani ya hali ya juu ajenge uhusiano na Mwenyezi Mungu na kutimiza haki yake vilevile kwa kupata khulka za hali za juu atimize haki za viumbe vyake na pia nilieleza kwamba wakati Mwenyezi Mungu Alipotuma Mtume saw kwa ajili ya kurekebisha dunia nzima na kwa ajili ya kupata lengo hili Mtume saw alifanya mahubiri na tena hakufanya mahubiri tu bali usiku kucha kwa ajili ya kupata matokeo alifanya maombi kiasi hiki kwamba alitoa machozi sana.Kwa ajili ya kurekebisha na kusalimisha binadamu uchungu aliokuwa nao moyoni mwake hatuwezi kueleza hali yake.Kwa kuona maombi yake Mwenyezi Mungu Alimwambia kwamba ikiwa watu hao hawakukubali na hawakuamini je utakufa?Lakini Mwenyezi Mungu kwa kusema hayo hakukaa kimya na hakurudisha maombi yake bali Aliyapokea maombi yake na Alileta utulivu kwa ajili yake na wale waliojizama katika maovu,kwa kuacha maovu wakawa wenye khulka njema na kujenga mahusiano mazuri na Mwenyezi Mungu.

Mabadiliko haya hayawezi kuletwa kwa kutumia nguvu ya dunia.Hii ilikuwa kazi ya Mwenyezi Mungu Ambaye Anapokea maombi na Anatawala mioyo ya watu. Kisha nilisema hii pia kwamba Mtume saw aliwatendea maadui vizuri kiasi hiki kwamba mfano wake haupatikani duniani kote. Maadui wale waliodhulumu sana katika Makka,wakati wa ushindi wa Makka Mtume saw aliwasamehe hivi kana kwamba hawakufanya kosa lolote wala hawakudhulumu.Kila kafiri alisamehewa kwa sharti hili kwamba atafuata sheria ya nchi. Kwa kuona hali hiyo maadui wakubwa waliozidi sana katika ukafiri walisema kwamba khulka hii inaweza kuoneshwa na nabii tu na kwa hivi wengine waliamini.

Nilisema hii pia kwamba katika kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Alimwita Mtume saw kuwa Rehema kwa walimwengu na Mtume saw alikuwa rehema ya hali ya juu,na mifano inayothibitisha kauli ya Allah iko maelfu ambayo inaweza kuelezwa. Na nilisema pia kwa kuwa na hali hii kwamba Mtume saw alikuwa rehema kwa ulimwengu,Islam na Mtume saw anashutumiwa kwamba walipigana vita na inasemwa hii kwa sababu ya kutokujua historia ya Islam.Mtume saw hakutangulia katika kuanzisha vita,katika mji wa Makka alidhulumiwa na kuteswa na wakati alipodhulumiwa kupita kiasi alihamia Madina lakini wakati wenyeji wa Makka waliposhambulia Madina, wakati ule Mwenyezi Mungu alijibu na hapo nilisoma aya ya Kurani Tukufu ambazo ni aya mbili za Sura Al Hajj ambamo Mwenyezi Mungu Anasema, imeruhusiwa kupigana kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa;nakwayakini Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kuwasaidia; Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu wanasema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu.Na kama Mwenyezi Mungu Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi. Na bila shaka Mwenyezi Mungu Humsaidia yule anayemsaidia Yeye; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mshindi; kama nilivyosema kwamba katika aya hizi waislamu waliruhusiwa kujilinda na vilevile waliamrishwa kulinda nyumba za ibada za watu wengine na Mwenyezi Mungu Anasema kwamba Ana uwezo wa kuwasaidia waislamu na makafiri licha ya kuwa na nguvu watashindwa na Mwenyezi Mungu Aliwapatia waislamu ushindi juu ya makafiri na makafiri walishindwa licha ya kuwa na silaha nyingi vilevile vita zilizopiganwa na makhalifa zilikuwa kwa ajili ya kuhakikisha amani na si kwa ajili ya kupata utawala nao walisaidiwa na Mwenyezi Mungu kama Alivyoahidi Yeye.

Katika hotuba yangu nilisema haya pia kwamba endapo waislamu wameenda mbali na dini na dhuluma inatendewa na waislamu basi hii ni sawa na bishara itolewayo na Mtume Muhammad saw. Ikiwa hali hii inapatikana basi sio maana yake kuwa huu ni mwisho wa Waislamu. Nina imani hii pia kwamba ikiwa bishara ya kupotea kwa waislamu ilitolewa na bishara ile ilitimia vilevile bishara ya kurekebishwa kwao pia itatimia na itatimia kwa kufika kwa masihi aliyeahidiwa. Na mimi nilisema kwamba mimi na jumuiya tunaamini kwamba yule masihi aliyeahidiwa ameshafika ambaye ni mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya na yeye ameyahuisha mafundisho ya dini tukufu ya Kiislam na kuanzisha jumuiya inayofuata mafundisho sahihi ya dini tukufu ya Islam. Na nilieleza hii pia kwamba Masihi Aliyeahidiwa as aliyekuja kwa kuhuisha dini, yeye pia alisaidiwa na Mwenyezi Mungu na kwa kueleza misaada ile nilieleza mifano kadhaa. Nilieleza bishara tatu kwa kuthibitisha ukweli wa Syedna Ahmad as, kwa mfano alisema Syedna Ahmad as kwamba katika zama hii matetemeko ya ardhi yatatokea sana na twapoangalia katika historia basi katika karne hii matetemeko yalitokea zaidi kushinda karne zote za zamani kisha bishara nyingine ielezwayo na Syedna Ahmad as ilikuwa kuhusu Zar aliyekuwa mwenyekiti wa Urusi atakamatwa na kuangamizwa,bishara hii pia ilitimia kisha bishara ya tatu aliyoieleza ilikuwa kuhusu vita kwamba tumekwishaona vita mbili kuu za dunia lakini dunia tena inaelekea upande wa vita ya tatu. Nchi zote zinaweka bajeti ya jeshi zaidi kuliko bajeti ya mahitaji mengine na kila nchi inaelekea kwenye kuongeza nguvu ya kijeshi. Ikiwa amani haipatikani duniani basi sababu yake sio dini bali sababu yake ni tamaa na siasa.

Nilisema hii pia kwamba katika zama hii aliyetumwa na Mwenyezi Mungu, msaada Wake pia unapatikana pamoja naye, ikiwa msaada wa Mwenyezi Mungu usingepatikana yule aliyekuwa anakaa katika kijiji kimoja cha Qadiyan asingeweza kufikisha ujumbe wake duniani kote kisha baada ya kifo cha Syedna Ahmad as nidhamu ya Ukhalifa ilianzishwa na kwa kupitia nidhamu hiyo kazi hii inaendelea kufanywa duniani kote. Ikiwa nidhamu hii inathibitisha kwamba Mwenyezi Mungu Yupo pia inathibitisha kwamba Mwenyezi Mungu Anasaidia Jumuiya hii.Nilisema hii pia kwamba Mwenyezi Mungu Ametupatia akili kwamba Mungu Yupo naYe Anaongea na waja Wake hivyo dunia inatakiwa kuelekea upande huu na isimlaumu Mungu kwa sababu ya makosa yao. Mwenyezi Mungu Aijaalie dunia iweze kufuata nasaha hizi, Huzur anasema huu ni muhtasari wa hotuba yangu niliyotoa kule takriban kwa nusu saa.

Sasa nitaeleza maoni ya baadhi ya watu kuhusu mkutano ule, watu walisema kwamba mafundisho ya dini tukufu ya Islam yaliyoelezwa yamewaathiri sana. Bi Stein Villumsted ambaye ni katibu mkuu wa shirika la viongozi wa dini katika Ulaya alisema, kujumuika hivi na kukaa pamoja na kuwasikiliza viongozi wa dini mbalimbali, kisha kukiri kwamba tunataka amani ni ufaulu mkubwa sana. Kisha mbalozi wa Grenada Mheshimiwa Joslyn Whiteman anasema kwamba sherehe hii ilikuwa nzuri sana. Wazo hili kwamba viongozi wa dini mbalimbali wanaweza kujumuika hivi limezidisha imani yetu na faida yake pia ni hii kwamba tunapata mwelekeo wa namna gani tunaweza kuwajumuisha watu kuhusu matatizo mbalimbali. Kamanda wa Metropolitan polisi London anasema kwamba kitu kilichomfurahisha zaidi katika sherehe hii ni kwamba kila

Endelea uk. 8

Mkutano wa dini zote uliondaliwa na Jumuiya

Kutoka uk. 4

mmoja ameeleza sifa za dini yake na hakuleta shutuma dhidi ya dini zingine, hii inaonesha kwamba sisi tupo pamoja.

Kisha kuna Bwana Charles Tannock ambaye ni mwakilishi wa bunge la Ulaya,yeye anasema kwamba siku za usoni sisi hatuna njia nyingine isipokuwa kufuata njia hii, sisi sote tunamwamini Mwenyezi Mungu na hatuwezi kuamini ya kuwa Mwenyezi Mungu Anataka kwamba kwa jina la dini tupigane hivyo mimi naunga mkono na ujumbe huu wa amani na ujumbe wa Jumuiya ninaopenda ndio huu kwamba,mapenzi kwa wote chuki si kwa yeyote, huu ni ujumbe wa ulimwenguni, kadiri viongozi wakiendelea kukaa pamoja itakuwa vizuri.

Bi Baroness Berridge ambaye ni mwenyekiti wa makundi ya wabunge wa Uingireza ya kutetea uhuru wa dini zote anasema, nina heshima ya kuwa mwenyekiti wa makundi ya wabunge wote,ninajua vizuri kwamba kwa namna gani Jumuiya ya Ahmadiyya inaendelea kutoa huduma zake kwa ajili ya kheri ya wengine na jambo hilo lilielezwa na Imamu wa Jumuiya pia. Sisi tunafurahi kwamba tunasaidiana pamoja na Jumuiya na ninafurahi kwa sababu hii pia Waahmadiyya wana uhuru katika nchi hii.

Kisha Bwana Katrigh ambaye ni mjumbe wa kamati ya wabunge wa vyama vyote ya kutetea uhuru wa dini alisema kwamba, Imamu wa Jumuiya aliyoyasema, inaonekana ya kuwa yanapatikana katika dini zote. Katika vyombo vya habari dini imeelezwa kuwa chanzo cha kuleta ufisadi kati ya binadamu lakini leo yale ambayo tumeyashuhudia hapa ni kinyume cha yale yaoneshwayo kwenye televisheni na katika vyombo vya habari.

Kisha Rabai alitoa ujumbe wake na maoni yake kwa kusema kwamba,ujumbe wa Imamu wa Jumuiya ya Ahmadiyya ni ujumbe wa amani na ujumbe wa kuelewana na tunapaswa kuheshimiana kwani sisi sote ni watoto wa Adam as, tunatakiwa kuishi kwa amani bila kupigana wenyewe kwa wenyewe. Bali kadiri tunavyoweza tunatakiwa tufanye juhudi kwa ajili ya amani.

Huzur anasema huyu ni rabai anatakiwa aifahamishe serekali yake pia kuhusu ujumbe huu.

Kisha kuna diwani Santok Singh yeye anasema ya kwamba kwa mtazamo wangu Imamu wa Jumuiya anatueleweshe kwamba katika dini zote mafundisho mengi yanafanana, dini zote zinatufundisha kuhusu ubinadamu, tunatakiwa tufanye kazi kwa pamoja, tunatakiwa tutakiane kheri.

Kisha kutoka Norwe kuna Bwana Billi Tanger ambaye anatokana na chama cha siasa anasema kwamba Imamu wa Jumuiya katika mwisho wa hotuba yake ametupatia ujumbe mmoja mzito kwamba tunatakiwa tufanye kazi kwa ajili ya amani na huu ndio ujumbe unaohitajika duniani siku hizi,na huu ndio ujumbe tunaotaka ufike Norwe pia.

Professa wa chuo cha Amsterdam aitwaye Daktari Sunias alisema kwamba Imamu wa Jumuiya alisema waziwazi kwamba mafundisho ya dini tukufu Islam badala ya ugaidi yatuhimiza kuhusu amani.

Kisha Bwana Aethelwine ambaye ni papa wa Greek Arthodox of Patriarchate Antioch,yeye alisema kwamba niliwahi kushiriki katika mikutano mingi ya Jumuiya,mimi napenda sana ujumbe wa Imamu wa Jumuiya,hotuba ya Kiongozi wa Jumuiya ilikuwa nzuri kushinda hotuba zote zingine,bila shaka kuwajumuisha viongozi mbalimbali hivi ni kazi inayostahili pongezi sana na vilevile ni ufaulu mkubwa sana.

Mgeni mmoja atokaye Ireland alisema,mimi nimeshiriki katika mkutano huu,ujumbe niliopata katika mkutano huu umenitetemesha,nawaambia wanajumuiya kwamba si rahisi kusambaza ujumbe huu bila kutumia vyombo vya habari,jumuiya inafanya kazi nzuri na nitafurahi ikiwa mtaweza kusambaza ujumbe wenu kwa watu.

Kisha kuna Jehangir Sarosh ambaye ni mjumbe wa shirika la viongozi wa dini la Ulaya anasema kwamba mimi nafuata dhehebu la Zoroastrian,nimefarijika sana kwa kuona sherehe ya leo. Viongozi wote walitoa hotuba nzuri lakini mwishowe hotuba ya Imamu wa Jumuiya ilikuwa nzuri sana.

Kisha kuna Bwana Robin Seiz ambaye ni mwalimu wa mafundisho ya dini anasema kwamba nilikuwa sitegemei kwamba nitapata raha na ladha kiasi hiki,nilisikiliza hotuba mbalimbali lazima baada ya kurudi nyumbani nitafikiria kuhusu hotuba hizi,nina yakini kuwa hotuba ya Imamu wa Jumuiya itachapishwa haraka iwezekanavyo.

Kisha Bwana Dk keni ambaye anahusika na kanisa la katoliki alisema kwamba muda fulani watu walianza kufikiria kwamba sisi hatuhitaji dini lakini hii imethibitika vizuri kwamba wazo hilo si sahihi na hauna msingi hata kidogo.

Kisha kutoka katika chuo cha Ubilgiji Bwana Dk Lidia na professa mwingine walikuja kwenye mkutano,wao walisema kwamba kwa kusikiliza hotuba ya Imamu wa Jumuiya ya Ahmadiyya iliyokuwa kuhusu mafundisho ya Islam na kurani Tukufu tumeathirika sana na baada ya kuisikiliza hotuba hiyo tumeamua ya kuwa tutawapatia wanafunzi tafsiri ya kurani Tukufu chuoni ili wao kwa kuisoma waweze kujua mafundisho sahihi ya kurani Tukufu,kwa hiyo Huzur anasema wao walipewa tafsiri ya kurani Tukufu na hivi njia za mahubiri pia zimefunguka kwa ajili yetu.

Santiago Qatariyubo aliyetokea Hispania naye ni professa katika chuo cha Madrid na ameandika vitabu vingi na ni rafiki wa jumuiya. Alishiriki katika mkutano uliofanywa huko Brussals Ulaya 2012 na alikutana nami pia,anasema,nikianza kueleza maoni kuhusu mkutano huu basi yanahitaji kurasa nyingi sana.Katika historia ya dunia dini ilikuwa sababu ya kuleta vurugu duniani hata katika zama hizi pia vurugu ipo kati ya mashariki na magharibi na kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea nah ii inaweza kuelezwa kuwa sababu ya kuleta vurugu duniani lakini kauli mbiu ya Jumuiya isemayo mapenzi kwa wote chuki si kwa yeyote ni muhtasari wa dini zote na wito huu unawajumuisha watu wote ambao wana mitazamo mbalimbali na katika zama hii ambamo kundi fulani la Waislamu linaungana na watu ambao wanashambulia na kueneza ufisadi,katika hali hiyo kazi ya Jumiya ni nzuri sana.

Inatakiwa sherehe ya aina hii ipate umashuhuri sana katika dunia nzima.

Bwana Garcia ambaye ni mwenyeji wa Pedro Abad Hispania alishiriki mkutanoni,aliwahi kuwa meya. Wakati alipokuwa meya mwaka 1980 alitoa ruhusa ya kujenga msikiti wa Albasharat huko Hispania na wakati wa ufunguzi wa msikiti huo alikutana na Khalifa Mtukufu wa nne na Khalifa Mtukufu wa nne alimpatia zawadi ya shahada baadaye aliweka zawadi ile ofisini mwake anasema kwamba Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya imewaalika wabunge,wanasiasa na watu wanaohusika na idara mbalimbali za binadamu,hao wote wamekusanywa katika mji wa London ili wafikirie kuhusu maelewano na kuhusu umoja nami naipongeza Jumuiya kwa kazi yao hii,nina hamu kwamba Jumuiya ifaulu katika malengo yake.Nina heshima ya kukutana na Khalifa wa Tatu alipokuja kuweka jiwe la msingi mwaka 1981 huko Pedro Abad na vilevile mwaka 1982 niliweza kukutana na Khalifa wa nne pia sasa katika mkutano huu nimepata bahati ya kukutana na Khalifa wa Tano.Mimi nimeathirika sana kwa kusikia maneno ya Mirza Masroor Ahamd ,amezungumza kuhusu jamii yenye amani na usalama na amepinga serekali ambayo kwa jina la kujilinda inatanguliza silaha juu ya ubinadamu.Nina fahari kwamba Imamu wa Jumuiya amewaalika viongozi kwa ajili ya kujenga jamii ambayo inaelewana,sisi tunaishi katika dunia ambayo ina mfarakano sana na watu wanakufa na njaa.Upande mmoja tunatupa chakula baharini na upande mwingine wako watu mamilioni ambao hawapati chakula,upande mmoja wapo matajiri ambao wana mamilioni na upande mwingine watu wanaendelea kuwa maskini zaidi,tunataka dunia ambayo inakataa vita na kutaka amani na kuwajumuisha watu wote katika maendeleo ambayo isimame dhidi ya dhuluma na kusambaza uadilifu.

Huzur anasema haya ni maoni kadha niliyoeleza,Mwenyezi Mungu Aijaalie kwamba dunia imwelekee Mwenyezi Mungu na kwa sababu ya kumtambua Mungu wanaweza kusalimika katika maangamizo ambayo yapo mlangoni mwa dunia na habari yake imetolewa na Syedna Ahmad as mara kwa mara.

Huzur alisema leo tena nataka kuwakumbusheni kuhusu wanajumuiya wa Pakistan muwaombee Mwenyezi Mungu Awasalimishe katika shari ya wote na Awasalimishe wale wote wanaopenda amani ipatikane nchini na hawataki ufisadi vilevile mufanye maombi kwa ajili ya Sirya,kule pia Mwenyezi Mungu Awalinde wanajumuiya,hivi karibuni mwanajumuiya mmoja alikamatwa tena bila kuwa na sababu yoyote,Mwenyezi Mungu Awalinde hawa wote na kwa jumla muiombee dunia hii kwa sababu hali inayopatikana duniani inaonesha kwamba wanaelekea kwenye vita lakini serekali zenye nguvu hazielewi ya kuwa wanaelekea kwenye shimo la maangamizo,ni jukumu letu kwamba sisi tuwaombee sana.

SHURA YA KITAIFA 2014

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwakumbusha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na kalenda ya matukio ya Jumuiya ya mwaka 2013/14 Majlis Shura ya Kitaifa itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam siku za Jumamosi na Jumapili tarehe 26 - 27 April 2013.

Matawi yote yanatakiwa yafanye vikao vya kupendekeza ajenda za Shura pamoja na kuchagua wajumbe wa kuyawakilisha matawi yao kwenye Shura hiyo ya Kitaifa.

Wajumbe wote wanatakiwa wawe wamefika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam jioni ya siku ya Ijumaa tarehe 25 April 2014.

Ni muhimu kila tawi la Jumuiya lisipoteze nafasi yake ya kuleta mjumbe pamoja na ajenda kama watakuwa nayo.

Bustani ya Washairi

Sanaa ya ushairi inawapa matatizo wanafunzi wengi mashuleni. Tumeamua kuwasasidia wanafunzi ili kujenga mapenzi ya sanaa hii na kuona ya kwamba mashairi ni sanaa ambayo ina utamu wa ajabu. Mwalimu Alli Seba Masamba ambaye amekuwa mwalimu wa somo hili kwa miaka mingi atakuwa anatuletea mfululizo wa mashairi ambayo pia yatakuwa na maswali na majibu. Katika toleo hili tunaanza na shairi "Ugeukapo wakati".

1. Wakati ni kitu chema, ukujiapo kwa heri
   Hukupamhiya neema, kwa laili na nahari
   Ukafurahi mtima, na uso ukanawiri
   Lakini ni mdahari, ugeukapo wakati

2. Wakati hujitukuza, na kufanywa mashuhuri
   Wendapo ukapendeza, kama anga la Gamari
   Huzagaa penye kiza, kwa nuru kutanawiri
   Lakini ni mdahari, ugeukapo wakati

3. Wakati hukupa kiti, cha ukuu na fahari
   Ukapanda kukiketi, na kupitisha amuri
   Pasiwe wenye sauti, wa kuweza kuusiri
   Lakini ni mdahari, ugeukapo wakati

4. Wakati una mazingo, kuzingakwe kuwaathiri
   Wenye mato huwa tongo, rijali akawa thori
   Mamboye huwa majongo, asiweze kushamiri
   Ndipo iwapo athari, ugeukapo wakati

5. Wakati ni kama taa, yenye muwali wa nari
   Kung'ara na kuzagaa, moyoni usikughuri
   Izimikapo ni baa, kizani hainawiri
   Na hino ndiyo athari, ugeukapo wakati

6. Wakati ungakukuza, kiumbe usijighuri
   Si mno kumsaliza, ambaye hutajabari
   Mara nyingi humsoza, mwenye kukosa nadhari
   Ikawa kumu khasiri, Igeukapo wakati

7. Wakati una khadhaa, wimapo ukashamiri
   Hudhania utakaa, zisigeuke dahari

   Lakini una nabaa, uzingapo hukhasiri
   Na hino ndiyo athari, ugeukapo wakati

8. Wakati ulipokwima, kwa wapi seo dahari
   Walisema haukoma, kupata kukawaghuri
   Mwishowe uliwatama, mengo yakataghayari
   Ikawa kuwaathiri, kwa kuzingakwe wakati

9. Wakati ni kitu chema, na ni kitu afkhari
   Na wendapo ukakoma, zigeukapo dahari
   Wa mbele kuwa wa nyuma, akawa hana shauri
   Lakini una athari, ugeukapo wakati

10. Wakati utizameni, muzikumbuke dahari
    Hukulaza masikini, ukaamka tajiri
    Na mlelewa malini, akaamka fakiri
    Na hino ndiyo khatari, ugeukapo wakati

Kifo cha mshairi huleta hisia kali kutoka kwa Mshairi. Kalamu ya mshairi humaizi hasara iliyotokea. Mistari idondokayo kutoka kwenye kalamu ya mshairi ni hazina ya taifa. Taifa hupata hasara na pengo lisilo zibika. Na pengo ambalo ni vigumu kuliziba. Mshairi wetu Mvumo ana kilio cha kuwapoteza wale waliohami ushairi. Ni beti zenye utamu wa ajabu. Ni za huzuni lakini ni sherehe katika utunzi unaofuata mila na desturi, muwala na mizani. Ni mistari ya johari, maneno mazuri yaliyopangwa vizuri hivyo kutoa furaha ya abadi, furaha ya mfuriko.

TWALIA UZIMBE ZIMBE

1 Tumepatika wasongo, wa mserego na dambe
  Machozi yazidi ungo, viswiswi hawana tembe
  Hai! Twakuuza dongo, waliko wetu wajumbe?
  Twalia uzimbezimbe, wawapi watunzi kongo

2 Walokuwa na miongo, isofumbizwa usimbe
  Shabani Fumo Lyongo, na Kaluta Seserumbe
  Hai! we mwenye majongo, umetutendaje kumbe?
  Twalia uzimbezimbe, wawapi watunzi kongo

3 Naya fuke maji shingo, na yagugume yasombe
  Mathias huwa mango, Khamisi kule akimbe
  Hai! wa leo viongo, yupi mgusa kikombe
  Twalia uzimbezimbe, wawapi watunzi kongo

4 Ni nani wale vigango, na ni nani wao jumbe
  Nambia vyao vitengo, na vyuo vyao vya shumbe
  Hai! Dunia u mwongo, asambe wetu asambe
  Twalia uzimbezimbe, wawapi watunzi kongo

5 Ulimwengu una chongo, kwa wakufunzi viumbe
  Unalo tumbo la chango, uonapo mtu rembe?
  Hai! Twalia kwa nyongo, kutuachia wazembe
  Twalia uzimbezimbe, wawapi watunzi kongo

6 Umesumburusha tumbo, hazina futu na lumbe
  Ni utusi wa utungo, unasomewa mzumbe
  Hai! Utupu ulingo, kiti hakina mpambe
  Twalia uzimbezimbe, wawapi watunzi kongo

7 Na kama mwenye malango, yupo aime atambe
  Tuone azibe pengo, la zingiti sio gombe
  Hai! Si hawa waengo, huvuta wakanywa pombe
  Twalia uzimbezimbe, wawapi watunzi kongo

8 Tamati maji ya tango, najinywesha nisiyumbe
  Eshi yale ya sifongo, yaliyopokutiwa wambe
  Hai! Nifute matongo, nambe dunia unambe
  Twalia uzimbezimbe, wawapi watunzi kongo

Adamu Najaso (Mvumo) - Lindi

Utenzi wa mwana kupona ni utenzi unaomuasa binti mambo anayotakiwa kufanya kwa mumewe. Shabaani Robert naye ameandika utenzi akimuasa binti yake kufuata njia iliyonyooka katika ndoa yake. Abdallah Khamisi Mbanga (Kungwi) katika kufuata nyayo za wakongwe hao waliopita kachukua kalamu ili kumuasi bintiye Sauda ashike njia iliyonyooka katika ndoa yake. Ingawaje shairi hili ni kwa Bi. Sauda lakini matumaini yetu ni kwamba litawafikia watu wengine. Kama methali ya kihaya inavyosema; 'Bagambila balinsi baliiguru kuulila'. Unawaambia wa chini na walio juu watasikia.

1 Sauda binti yangu, leo umepata mume
  Umefunga njema pingu, ni suna yake Mtume
  Nakupa pongezi zangu, hongera mwana uneme
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

2 Mwali wangu nakufunda, kwenye ndoa usikwame
  Kwa lugha ya tafsida, mambo machache niseme
  Ndoani kuna agenda, inabidi uzisome
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

3 Mama nakupa mizungu, mimi kungwi wa kiume
  Jiepushe na usungu, kwa kumdharau mume
  Kapewa hadhi na Mungu, katukuzwa na mtume
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

4 Kumthamini mumeo, kwako awe Mfalme
  Kwako ndio mwenye cheo, wengine magumegume
  Chonde usimpe ndweo, ukafanya ajiume
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

5 Sauda kafanye twaa, hata zama za ukame
  Liwe dona kwa dagaa, tafuna usilalame
  Mola tawapa wasaa, riziki njema mchume
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

6 Amka alfajiri, mbilini usikorome
  Weka maji ya uturi, umwandalie mume
  Kwenye sala na dhihiri, kidete ukasimame
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

7 Mume anataka fani, ili kwako atuame
  Mpapase maungoni, kifuani muegame
  Na anapokutamani, usingoje akutume
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

8 Mumeo ukamuenge, kwenye mahaba azame
  Sio ukawe mawenge, utakuja akuhame
  Penzi nenda kalijenge, majirani waachame
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

9 Anaporudi nyumbani, umpokee kwa shime
  Muulize kulikoni, yalomsibu aseme
  Kisha kwa lugha laini, mliwaze wako mume
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

10 Mnapokuwa wawili, kwa mapenzi mtazame
  Akushikapo pa mwili, legea usikakame
  Mwaya zingatia hili, ndoa yako usileme
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

11 Ukawe ukijichunga, heshima ndugu wa mume
  Ukaziepushe ngenga, za kuwaudhi wa kilume
  Ndoa yako bado changa, nenda kaitometome
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

12 Tena usimangemange, majiani siyoyome
  Na safari usipange, omba ruhusa ya mume
  Akigoma usipinge, nyamaza usilolome
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

13 Ukabaki njia kuu, michepuko ikukome
  Namwomba Mungu Mkuu, ndoayo aitazame
  Nipate na wajukuu, wa kike na wa kiume
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

14 Tarehe kumi na nne, Machi kwako ni ya shime
  Beti ya kumi na nne, nitakukabidhi mume
  Ukampe dozi nene, daima asikuteme
  Sauda heshimu mume, ana sifa ya Mtume

Abdallah Khamisi Mbanga (Kungwi)
Tambani mkoani Pwani

HUMZIZIMA BARIDI

1 Karatasi nakutuma, ufike kila biladi
  Ukishafika salama, usichelewe kurudi
  Hadithi hii nasema, ya kondoo na baridi
  Humzizima baridi, kwa mwenye manyoya haba

2 Kama manyoya si haba, yanajaa chungu nzima
  Japo ipite dhoruba, na baridi ya kuvuma
  Kondoo halii toba, na hawezi kutetema
  Baridi humzizima, kwa mwenye manyoya haba

3 Kondoo akilalama, wala hafanyi kusudi
  Manyoya yamemhama, na upepo umezidi
  Hapo huona nakama, lakini hapana budi
  Humzizima baridi, kwa mwenye manyoya haba

4 Yule alojaa tele, mwilini yamtitima
  Huenda huku na kule, hudharau hata ndama
  Hudhani wenziwe wale, wenyewe wamejinyima
  Baridi humzizima, kwa mwenye manyoya haba

5 Yule asiye manyoya, hupunguzika idadi
  Kutwa anawayawaya, hudharau hata jadi
  Anajitoa hadaya, akidhi wake mradi
  Humzizima baridi, kwa mwenye manyoya haba

6 Mwenye manyoya hutamba, hasa awe kwenye boma
  Hujiona kama simba, huku akiunguruma
  Hutaka vaa kilemba, kuusahau unyama
  Baridi humzizima, kwa mwenye manyoya haba

7 Mwenye manyoya shufufu, mengi anayafaidi
  Hupungukiwa na bifu, haogopi hata radi
  Huvimba vimba minofu, mfano wa tembo budi
  Humzizima baridi, kwa mwenye manyoya haba

8 Mwenye manyoya machache, mengi yanamsakama
  Huogopa hata cheche, kidogo ikiwa homa
  Japo na apafikiche, ngozi hupata alama
  Baridi humzizima, kwa mwenye manyoya haba

9 Kondoo hajisifii, manyoya kwake zaidi
  Na hata hajivunii, hakuomba ila sudi
  Ila kwa dunia hii, lazima iwe hasidi
  Humzizima baridi, kwa mwenye manyoya haba

10 Naomba kwake Wadudi, unijalie salama
  Ingawa nimeahidi, gazetini sitahama
  Lakini umenizidi, mwenzenu utu uzima
  Humzizima baridi, kwa mwenye manyoya haba

Sihiyana Salehe Mandevu (Mtenda wema)
Buguruni – Dar es salaam

Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.a.w

Ustadhi *A .R. Mikila – Morogoro*

Kutoka toleo lililopita

NDOTO ZA MTUME MUHAMMAD (SAW).

Historia inaonyesha kuwa, harakati za vuguvugu la**Tablighi** (mahubiri ya dini), ndani ya Makka na nje ya Mkka, zilipamba moto na kushika kasi kubwa, baada ya Mtume (saw) kupata ndoto hizi za Mi'raji na Isra. Huu ni ukweli wa kihistoria wa dini ya Islam na Maisha ya mtume Muhammad (saw).

MASWALI MUHIMU YA KUJIULIZA.

Hebu twende mbali kidogo katika tafakuri. Tujiulize, hivi safari hii ya Isara, ilikuwa na umuhimu gani kwa Mtume (saw)? Nini hasa yalikuwa makusudio ya safari na nini faida yake? Uislamu ulipata nini kwa safari ile?

Maswali hayo na mengine yote yanajibiwa na Qur'an Tukufu kwa mukhtasri wa ay hii:-

" Utukufu ni wa Yule Ambaye Alimpeleka Mtumishi wake usiku, kutoka Msikiti Mtukufu (Makka) mpaka Msikiti wa Aqsaa ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake, ili Tumuonyeshe baadhi ya ishara Zetu. Hakika Yeye Ndiye Asikiaye Aonaye" (Kur, 17:2)

Kwa mujibu wa Aya hii, madhumuni ya safari ya Isra, yalikuwa ni kumpeleka Mtume (saw) Masjidi Aqsaa ili akaone Ishara za Mwenyezi Mungu na vitu vilivyo barikiwa vilivyopo kule. Ishara hizo na vitu hivyo vinatangaza utukufu wa Allah. Pia kumthibitishia kuwa Alla Anasikia na Anaona. Sifa za Allah za **kusikia** na **kuona** zimetiliwa mkazo katika aya hii, ili kujenga taswira ya umuhimu wa safari ile.Tujiulize! Mungu Alisikia nini, na Aliona nini chenye faida kwa Mtume (saw) na uislamu kwa ujumla, hata Alazimike kumpeleka Mtume Wake Masjidi Aqsaa usiku?

Mpendwa msomaji wangu, makala hii inakusudia kukutoa gizani kwa kukudokezea yale ambayo Allah aliyasikia na yale Aliyo yaona kabla ya kufanyika kwa safari hii ya Isra, na yale yaliyojiri baada ya kufanyika kwa Isra.

Kwanza ifahamike kuwa, neon 'Masjidi'au'msikiti' linatumika kuashiria jengo la ibada linalo tumiwa na waislamu. Neno hili halitumiki kwa majengo ya ibada za dini nyingine. Kutumika kwa neno Masjidi Aqsaa (Msikiti wa mbali) kulikusudia kudokeza kwamba Mtume (saw) atakuwa kiongozi wa Misikiti miwili mitukufu(*Haramain*). Sinagogi la kale, Jengo la ibada lililo jengwa na Nabii Sulaimani kule Jerusalemu, si miongoni mwa Haramain. Qur'an haikukusudia kutaja habari za Sinagogi lile ambalo kimsingi halikuwa na vitu vyovyote maalum vya kuhitajika Mtume (saw), asafirishwe usiku kwenda kuviona. Kama kungelikuwamo vitu hivho muhimu, basi angesafirishwa mchana kweupe, tena siyo peke yake, bali pamoja na masahaba zake;. Kulikuwa hakuna kipingamizi chochote kwa Allah kufanya hivyo. Mbona akina Abu Sufiyani, ki na Walidi bin Mughira na wengineo wengi, walikuwa wakienda kule na kurudi kule wakifanya biashara?

Uhakika hasa wa mambo ni huu kwamba, Safari ya **Isra** ilikuwa ni onyesho la kiroho tu, lenye makusudio makuu mawili. Moja ni kumpa kibali Mtume (saw), cha kuihama Makka na kwenda kuishi Madina. Kibusara lilikuwa ni jambo la lazima kumuandaa kisaikolojia juu ya uhamisho huu mkubwa ulio mbele yake, wa yeye na wafuasi wake. Pia kumpa muda wa kutosha wa maandalizi. Walitakiwa kuihama Mkka na kwenda nchi ya mbali kwa nia ya kwenda kufanya kazi ya kueneza uislamu na kufanya ibada ya Mungu mmoja kwa uhuru zaidi na kwa upana mkubwa.

Shabaha ya pili ya **Isra** ilikuwa ni kuwaambia Maquraishi wa Makka, Islamu haikuja kwa ajili yao pekee, bali ni kwa ajili ya watu wote wa dunia hii na wa zama zote. Kwa hiyo upinzani wa wao na wa marafiki zao, dhidi ya uislamu ni kupoteza wakati bure. Allah Ndiye Mfalme Mwenye nguvu na Mwenye hekima kuliko wao. Tayari amemsikia mtume Wake akiomba kuhamia Madina na tayari Amezisikia kauli za watu wa Madina wakimuomba Mtume (saw) ahamie kwao. Amesikia kiapo chao pale Akaba katika mbonde la Minna kwamba wapo tayari kumlinda hata kufa kwa ajili yake. Pia Amesikia azimio lao Maquraishi, lile la kutaka kumuua Muhammad mtume Wake. Azimio walilopitisha kwenye vikao vyao vya siri ndani Daru nadwa. Kadhalika Mwenyezi Mungu, ameona haja ya kumuhamisha Mtume Wake, na kwamba wakati ulifika wa kumtoa Makka na kumpeleka Madina. Kwa kufanya hivyo, atakuwa katoa nafasi ya kupanuka kwa uislamu na kukomesha jeuri na majigambo ya bure ya viongozi wa Makka. Pia mwenyezi Mungu aliziona nafsi za mahasimu wa uislamu wa Makka, zina uchu wa kuua kwa kila hali hata ikibidi kupigana vita.



Ustadh Abdulrahman Mikila

Wasomao histoia ya maisha ya Mtume Muhammad (saw), watakubaliana nami kwamba, **ndoto hii ya Isra** ndiyo iliyo mchochea kwa kiasi kikubwa, Mtume (saw), kuifikiria zaidi Madina kwamba, ndiyo mahali pekee salama pa kuhamia na kufanya mahubiri na kueneza uislamu. Kwa sababu hiyo ndiyo maana alianza kufanya maandalizi ya kuihama Makka.

MAANDALIZI YA KUIHAMA MAKKA.

Katika mwaka wa nane wa utume, hali ya mateso dhidi ya waislamu iliongezeka maradufu na kuwa makubwa mno. Hata hivyo, Mtume (saw), hakukata tamaa aliendelea tu na kazi yake ya mahubiri. Alienda hapa na pale, mara kwa huyu mara kwa yule yule. Siku moja katika wakati Haji, akiwa katika maeneo ya Minna, kwa bahati tu, alikiona kikundi cha watu sita au saba hivi, wenyeji wa Madina. Mtume (saw), alikiendea kikundi hiki na kuomba kuongea nao. Watu hawa wakamkubalia ombi lake. Basi, aliongea nao na kuwaelezea ujumbe wa Allah alioteremshiwa. Akawaomba waupokee na kuwapelekea jamaa zao warudipo Madina. Pia aliomba kujua, iwapo watakuwa tayari kuwapokea baadhi ya waislamu wakipenda kuhamia Madina! Watu hawa walikuwa wa kabila la Khaziraji, kabila ambalo lilikuwa rafiki na Bani Qainuka Wayahudi wa Madina. Baada ya mazungumzo marefu na ya kina juu ya ujumbe ule mpya wa Islamu. Watu hawa walisilimu na kuahidi kuwa, wakirudi Madina wata waambia na ndugu nzao na jamaa zao juu ya Islam na mafundisho yake. Ama la kuhusu kuwapokea au kutowapokea waislamu watakao penda kuhamia Madina, hili waliahidi kutuo jibu katika Haji ijtakayo fata mwakani.

Watu hawa walipofika Madina, walifikisha ujumbe ule kwa ndugu zao. Watu wengi waliupoke kwa shangwe la ajabu. Ndugu hawa wakaanza kuhamasisha wenzao kukubali kufata mafundisho yale mapya ya Islamu, na kuacha tabia za ugomvi na uhasama usiokuwa na mwisho. Wakanadi kuwa, sasa wanapaswa kuungana na kuwa wamoja, chini ya kiongozi mmoja wa kijamii wa makabila yote ya waarabu wa Madina. Kutokana na ushauri huu na joto lile la hamasa, haraka wakafanya uchaguzi. Abdallah bin Ubay bin Salul akachaguliwa kuwa Kiongozi wa kwanza wa Makabila ya Ausi na Khazraji kule Madina. Kikundi hiki pia kiliweza kuhamasisha watu wengi kwenda Makka kuonana na Mtume (saw).

Haji iliyo fatia kikundi cha watu 12, kilisafiri kwenda Makka kwa nia ya kuonana na Mtume (saw). Watu hawa walipofika Makka na kuonana na Mtume (saw), walisilimu na kushikana mkono na Mtume (saw) na kutangaza utii (*baiyati*) wao kwake. Waliahidi kuacha maovu yote na kuacha kuabudu masanamu. Walipo rudi Madina waliongeza joto la hamasa kwa wengine. Watu walianza kukusanyika kwao kwa wingi na kuulizia habari za Mtume (saw), na waliulizwa mengi juu ya ya Islamu. Mahaji hawa walielemewa na maswali, walijitahihidi kujibu saw na uwezo wao, lakini mengi yaliwashinda. Hali hiyo ikawasukuma wapeleke ombi kwa Mtume (saw) ya kupatiwa mwalimu wa kuwafundisha uislamu. Mtume (saw) aliwapelekea Musaabu (r.a), mwalimu kuwafundisha Islamu na maarisho yake.

Katika Haji ya tatu kundi lingingine kubwa zaidi la watu 73, wanafunzi wa Musaabu (r.a), likiongozwa na bwana Al-Bara, lilifika Makka. Wao Walifika kwa nia moja tu, nayo ni kuongea na Mtume s.a.w, na kumuomba akubali kuhamia Madina. Walisema kwamba watu wa Madina, wanamtaka sana akakae nao na awe kiongozi wao. Mtume (saw), kimsingi Mtume (saw) hakuwakatalia ombi lao, wala kuwakubalilia moja kwa moja. Mtume (saw) alilimwita baba yake mdogo bwana Abbasi bin Abdul Mutwalib, kuja kusikiliza kauli ya watu wa Madina. Wakiwa katika bonde la **AKABA** mbele ya Abasi, kundi hili lilifunga ahadi kwamba, iwapo Mtume (saw) atakubali kuhamia Madina, wao na jamaa zao, watamlinda kikamilifu. Hawata muacha adhuriwe na adui yeyote yule. Watajitolea kwa hali na mali kumlinda hata ikilazimika kutoa uhai wao.

Huu ndiyo utukufu wake Allah, Aliouandaa na kutaka Mtume (saw), aende akauone mara atakapofika Madina.

" Utukufu ni wa Yule Ambaye Alimpeleka Mtumishi wake usiku, kutoka Msikiti Mtukufu (Makka) mpaka Msikiti wa Aqsaa ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake, ili Tumuonyeshe baadhi ya ishara Zetu. Hakika Yeye Ndiye Asikiaye Aonaye" (Kur, 17:2)

Joto la mabadiliko lililo ikumba Madina halina mfano. Wayahudi walioishi Madina na kuhubiri kwa karne nzima walishangaa na kuchanganyikiwa. Iweje wao walikuwa wakwanza kufika Madina kuhubiri **Tauhidi** tena kwa weledi sana, lakini hawakupata mafaniko chanya. Wala mahubiri yao hayakuwa na athari ya kuleta mabadiliko ya wazi kiasi cha kuiteka Madina. Walijiuliza ni muujiza gani huu, alio kujanao huyu Mtume wa kiarabu? Hali ile haikuwa habari njema kwao na wala haikuwafurahisha.

Baada ya **mkataba ule wa Akaba** kuridhiwa, siku chache zilizo fatia Mtume (saw), akapata ndoto hii tukufu ya **Isra**. Akajiona anasafiri kutoka Makka kwenda **Masjidi Aqsaa** (Jerusalemu) na alipofika kule akawasalisha Mitume wa zamani.

Kumbe kule kuridhia kwake kuhamia Madina, ndiko kuliko mithilishwa kindoto, kuwa anasafiri kwenda **Baitul Muqadasi,** kwenye mji wa wayahudi wenye nyumba ya ibada kwa lakabu ya **Masjidi Aqsaa.** Kindoto mji wa Madina umemithilishwa na **Baitul Muqadasi.** Mara alipofika Madina, Mtume (saw) alipewa uongozi wa kuingoza Madina na watu wake. Kindoto uongozi ule ulimithilishwa na uimamu wa kuwasalisha Mitume wote wa zamani pamoja na wafuasi wao. Mtume (saw) alipofika Madina aljenga msikiti wa ibada ya Mungu mmoja, **Masjidi Nabii**. kindoto msikiti ule ukamithilishwa na **Masjidi Aqsaa**. Masjidi Nabii ule wa Madina ndiyo uliyo mbali na Masjidi Haram wa Makka. Leo tujiulize je, waislamu wanapo enda kuhiji Makka, na kule Jerusalamuwanaenda? *Tafakari*.

Kule Madina yalikuwapo makazi ya Wayahudi bani Kuraiza, bani Qainuka na Bani Nadhir wote hao walikuwepo kule. Hao ni waalimu wa Ahalul Kitabu warithi wa **Masjid Aqsaa.**

Inasemekana kuwa wayahudi wale, walitoka makwao na kwenda kuishi Madina, kwa nia ya kumzaa nabii mfano wa Musa. Tabiri nyingi ndani ya Taurati yao zilionyesha kuwa Musa atazaliwa kwa mara ya pili; lakini katika nchi ya Parani (Kumb; 18:18). Kwa sababu hiyo, ndiyo maana Mtume (saw) ndani ya ndoto alionyeshwa kundi la wayahudi

Endelea uk. 8

Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.a.w

Kutoka uk. 7

hawa wa Madina kwa sura ya **Masjidi Aqsaa ya Jerusalemu.** Madina ndiko anako kusudiwa kupelekwa na kwenda kuishi.
Ni dhahihiri **Isra** ilitabiri mgongano huu, wa mafundisho ya dini hizi mbili, zinazo amini juu ya Tauhidi**.** Alitakiwa aende Madina akawahubiri Wayahudi kinadhraria na kimatendo. Alijenga Msikiti Madina (Masjidi Aqsaa) kwa lengo la kusimamisha Tauhidi ya kweli, isiyo na mawaa wala ubaguzi ndani yake, kama alivyo ona katika ndoto anawasalisha Mitume wengi waliokufa zamani.

Ili kuwakabili Wayahudi hawa wenye mafundisho ya Taurati na kuwasilimisha, aliwaambia:-

"... Ikiwa ninyi mwampenda Allah, basi nifuateni, Allah Atawapendeni na Atawaghufirieni madhambi yenu; na Allah ni Mwenye ghufira Mwenye rehema.. Enyi watu wa Kitabu njooni kwenye neon lililo sawa naina yetu na baina yenu,ya kwamba hatuta mwabudu yeyote ila Allah,walahatutamshirikisha na cho chote,wala baadhi yetu hatutamfanye wengine kuwa waungu badala ya Allah…" (3:32,65).

Ile aya ya Qur'an Tukufu , iliyomo ndani ya surat Jumaa iliyoshuka Madina isemayo:-
"Enyi mliyo amini! Inaponadiwa kwa ajili ya sala siku ya Ijumaa, basi nendeni upesi kumkumbuka Allah na acheni biashara; hiyo ni bora kwenu ikiwa mnajua" (Kur 62:10)

Aya hii iliyowaita watu wote waliosilimu kwenye ibada, bila kujali kabila wala rangi wala lugha ya mtu; ilidhihirisha wazi kuwa **Masjidi Nabii, ndiyo muwakilishi halisi wa ile Masjidi Aqsaa** ya kule Jerusalemu. Adhana ya kuita watu katika sala ya jamaa ilipatikana Madina (Jerusalemu mpya). Haya yaliyofanyika katika mji wa Madina mbona hatuyakuti ndani ya vitabu vya historia kwamba, yaliwahi kufanyika kule Jerusalemu. Vitabu hivyo wala havitaji chochot kuhusu tukio lile la kushuka usiku wala mchana, manabii wote wazamani na kufanya sala ya pamoja ndani ya masjid Aqsaa.
Matendo yote yanayotajwa ndani ya **safari ya Isra** hayajawahi kutendeka hata tendo moja, kule Jerusalemu ya Yuda; bali yote yalitendeka Madina.
Msomaji wangu mpendwa, kwa ushahidi wote huu nilio utoa, naamini utakuwa umekuwezesha kutambua kuwa **Masjidi Aqsaa** hasa, ni ule msikiti uliyo ujengwa na Mtume (saw) kule Madina, uitwao **Masjidi Nabii.**

Isra ilitabiri kwamba, safari ya Mtume (saw), kuhama Makka kwenda Madina itakuwa ya ghafla nay a siri kubwa; safari itakuwa ya usiku. Katika ndoto ya **Isra** Mtume (saw), alifatana na Malaika Jibril kama vile alivyo fatana naye katika safari ya Mi'raji. Malaika huyu ni swahiba wake wa muda Mrefu. Ndivyo ilivyo kuwa, katika safari yake ya kuhama Makka kwenda Madina, Mtume (saw) alifatana na Sayidina Abu Bakari Sadiq (r.a) rafiki yake kipenzi wa muda mrefu sana. Sayidina Abubakari ndani ya **safari ya Hijra** anaonekana kama Maalaika Jibrili kwa kumfariji Mtume (saw) safarini.

Ndani ya Madina (**Jerusalemu mpya**) uislamu ulipata maguruduma ya kutembelea na ya kukimbilia. Ndani ya Madina Mtume (saw), alipata uongozi wa ziada, (ufalme) wa kuingoza Madina na watu wake wote. Kwa hakika huu ndiyo ule uimamu aliopewa ndani ya **safari ya Isra** wa kusalisha manabii wenzake walio mtangulia. Katika sala ile aliwaongoza Manabii wote na wafuasi wao. Tendo lile lili kuwa ni kuonyesha kuwa, mafundisho ya Islam yatakuwa kwa ajili ya walimwengu wote na wa zama zote.

Katika **ndoto ya Isra,** Mtume (saw), alijiona anarudi kuelekea Makka na njiani alionyeshwa baadhi ya misafara ya biashara ikirudi kutoka Sham. Hivyo ndivyo ilivyo kuwa siku ile, Mtume (saw), alipo kuwa anaingia katika mji wa Makka akitokea Madina, aliongozana na msafara wa askari 10,000 pamoja naye.
"Yeye ndiye Aliye mtuma Mtume Wake kwa muongozo na kwa dini ya haki, ili kuifanya izishinde dini zote, japokuwa makafiri wachukie" (Kur; 61:10).

Kwa hakika huu ulikuwa ni ushindi mkubwa, dhidi ya makafiri wa Maka na marafiki zao.

3 - SAFARI YA KUTUFU KAABA.
Katika mwaka wa sita Hijiria, miezi michache baada ya vita vya handaki, Mtume (saw) aliota ndoto, akajiona yuko Makka na Masahaba zake anatufu Kaaba. Ndoto hii, aliipata katika mwezi wa Dhul-qaadi, mwezi uliyo miongoni mwa miezi ya Haji. Alipo amka asubhi aliwatangazia Masahaba zake kuwa, ameota ndoto anatufu Kaaba pamoja nao. Bila shaka hii ni ishara kwamba Mwenyezi Mungu anawataka waende Hija. Kwa hiyo aliwataka wajiandae kwa safari ya Haji, Masahaba 1500 walijiandaa kwa safari hii.

Qur'an Tukufu juu ya ndoto hii ikasema:-
"Kwa yakini Allah Amemhakikishia Mtume Wake njozi kwa haki; Bila shaka ninyi mtaingia katika Msikiti Mtukufu Inshaallah kwa salama, mkinyoa vichwa vyenu na kupunguza nywele, hamtaogopa na (Allah) Alijua msiyoyajua, na kabla ya haya Aliwapeni ushindi uliokaribu" (48:28)

Kwan bahati nzuri ndoto hii, haina utata wa tafsiri wala wa kukubalika kwake. Waislamu wote kwa jumla wanakubali kuwa Mtume (saw), kujiona anatufu Kaaba pamoja na masahaba zake, ilikuwa ni katika hali ya kindoto tu.

Kutokana na vita za mfululzo za miaka sita, waislamu walikuwa hawajawahi kwenda Makka kufanya Tawafu katika Kaaba. Kwan hiyo tangazo hili la kuwataka wajiandae kwa safari ya Hija, lilipokelewa kwa hamu kubwa na shauku sana.

Ndoto hii kwa nini inakubalika kiurahisi hivi, na hali zile zingine mbili hazikubaliki kwa shangwe la namna hii? Muota ndoto ya **Mi'raji, ndoto ya Isra na hii ya Kutufu Kaaba** ni mtu Yule Yule mmoja, yaani Mtume (saw)! Iweje basi baadhi ya waislamu wazichukulie safari zile za **Mi'raji na Isra** kuwa si ndoto, bali ni safari halisi za kimwili na kuibagua hii?
Jibu lake ni jepesi tu kwamba, ndoto zile mbili zilimtaja Mtume (saw) peke yake bila ya masahaba kushiriki katika safari zile, kwa hiyo ilikuwa ni rahisi kwa watu wa baadae kupindisha ukweli na kuzitangaza kuwa zilikuwa ni safari halisi za kimwili badala ya kuwa ndoto. Watu wapenda visa na mikasa kwa jazba wakadakia wakashabikia na kueneza masimulizi mchanganyiko. Masahaba wa Mtume (saw) kamwe hawakuwahi kuamini hivyo. Watu hao walichanganya haki na batili na kuicha haki na hali wanajua.
"Na msichangaje haki na batili, na mkaficha haki na hali mnajua"(Kur;2:43).

Pamoja na kwamba ndoto hii, inakubalika na waislamu wote, lakini si watu wengi wanao fahamu hakika yake na yale yaliyo jiri baada ya ndoto hii. Kwa sababu hiyo, nimeona ipo haja nisimulie japo kwa uchacheki, kwa faida ya hao wasiyo fahamu, na kwa wale walio sahau kuwarejeshea kumbukumbu ya ndoto hii.

CHANZO NI VITA VYA HANDAKI
Katika vita vya Uhudi, waislamu walishindwa. Wengi waliuawa na wengi walijeruhiwa, akiwamo Mtume (saw). Makafiri wa Makka waliifurahiya hujuma ile na kujitangazia ushindi kwa majigambo na bashasha sana kwamba, Mungu wao Hubali amemshinda Mungu wa Muhammadi (Astaghafirullah). Kauli hii ya kufuru na ya kifedhuli ilikuwa ni ya Abu Sufiyani, kiongozi wa Makafiri wa Makka katika vita ile. Kauli hii, haikuachwa ibaki bila majibu kutoka kwa Allah.

Ndipo baada ya mwaka mmoja kupita Mwenyezi Mungu Akafanya mpango wa kujibu fedhuli ilekwa namna ya ajabu kabisa. Baadhi ya makafiri wa Makka wakishirikiana na Wayadudi wa Madina, wakaanzisha choko choko upya ya kutaka kurudi tena Madina kivita. Kwenda kufanya shambulio kuu na la uhakika, waliona ushindi ule wa Uhudi haukutosha na haukuwa mnono. Waliona kwamba madhali Mtume Muhammadi (saw) na sahaba AbuBakari, Umari Uthumani na Masahaba wengine mashuhuri bado wangali hai, ni Muhali Makka kutulia. Wakaona ipo haja ya kurudi tena Madina kushambulia kimaangamizi na kuwaua mashujaa wote wakiislamu pamoja na Mtume (saw).

Kwa sababu hiyo mipango ikapangwa. Jeshi kubwa la askari 24,000 la makabila mchanganyiko, likakusanywa kwenda kuivamia Mdina. Mpango huu wa uvamizi wa jeshi hili kubwa la Makafiri, ulijulikana mapema. Kwa hiyo waislamu kwa upande wao na wao waka jitayarisha kumkabili adui. Kwa ushauri wa sahaba mmoja, Salman Farsy, alio utoa kwa Mtume (saw) walichimba handaki la kujihami lenye mtaro mrefu kuzunguka uwanja wa vita. Vita hii ikaja julikana kwa jina la **vita vya Handaki**. Huu ulikuwa ni msaada maalum kutoka Mbinguni. Wakati wa vita ulipowadia mbinu hii ngeni ilifanya kazi kubwa, iliweza kuzuia uvamizi ule hasidi usifanikiwe. Msaada mwingine wa kimbingu ulipatikana kutoka kwa bwana mmoja aliye itwa Nuaimu. Muungwana huyu mwenye huruma, alitokea katika jeshi la Makafiri ya Makka. Bila kuwasiliana na waislamu, Bwana huyu akatumia ujanja wake binasfi wa kuwavuruga kimawazo, viongozi wa Makka na maswahiba zao wa Madina banu Quraiza, Wayahudi. Hawa waliombwa na Viongozi wa Makka washirikiane kivita dhidi ya waislamu. Kwa husuda Wayahudi hawa wakakubali, huku wakijua kuwa wanayo makubaliano na Mtume (saw) kusaidina wakati wahatarikama ule. Bwana Nu'aim, alipojua hilo, alienda kwanza katika ngome ya wayahudi, akawatia hofu kwamba makubaliano yao na watu Makka ya kutaka wafanye mashambulizi ya pamoja dhidi ya waislamu si ya kuaminika. Aliwauliza hali yenu itakuwaje mbele ya Mhammadi, iwapo majeshi ya Makka yatakimbia mara mkisha anzisha mapigano? Si mtastahili lawama na hukumu dhidi yenu. Kisha akawashauri kwamba iwapo wapo tayari kufanya hivyo, ni heri basi waombe rehani kutoka kwa viongozi wa Makka ya watu sabini. Hawa muwashikilie, na toeni udhuru wa kuwahitaji watu hao kwa ulinzi wa masikani zenu; wakati ninyi mtakapo kuwa katika mapigano. Wayahudi wale waliona mantiki ya ushauri huu, wakapeleka ombi hili kwa viongo wa Makka. Kisha bwana Nua'im, akaenda kwa viongozi wa jeshi laMakka. Lilipo letwa ombi lile la kuhitaji watu wa kutolewa kuwa rehani, akawashauri viongozi wa Makka kuliktaa kwa madai kwamba Wayahudi wanaweza kuwasaliti watu wao kwa kuwakamatisha kwa Mtume (saw). Kama wao ni wakweli katika kushirikiana nasi kuna haja gani ya wao kutanguliza sharti hili? Kinacho takiwa ni wao kuanza tu mapigano. Si mnajua kwamba, hawa banu Quraiza wana makubaliano ya kushiriaka na Waislamu, je tukiwapa watu hao sabini tunauhakika gani juu ya usalama wao, si tutawangamiza watu wetu? Kwa njia hii kila upande ukaingiwa na hofu na kuto aminiana. Mbinu ya bwana Nu'aim ikausambaratisha ushirika huu hasidi.

Msaada wa mwingine kutoka kwa Allah ulikuwa ni Tufani la usiku wa siku ya kumi na kisa. Siku hiyo upepo mkali wa kudra ulizuka, ulivuma kwa kasi kubwa na ya ajabu. Upepo ule ulivunja mahema yote ya jeshi la makafiri na kuyatupa mbali. Sufuria zao za kupikia vyakula zilisukumwa na kupinduliwa, vijinga vya moto vilivyo kokwa mbele ya kila kambi vilirushwa huko na kusambaratika, vingi vikazimika. Hii kwao haikuwa dalili nzuri, bali ni ishara mbaya na mkosi, ishara ya kushindwa vita. Kwa sababu kwa imani yao, kuwasha moto na kuuweka mbele ya kila kambi ya maaskari, ulitakiwa moto huo kuwaka kwa kudumu uskiku kucha bila kuzimika. Hali hiyo iliaminika kuwa ni dalili ya sudi na ushindi kivita. Tukio hili la ajabula la kuzuka upepo wa kiasi kile na myoto yote kuzimika kwa kishindo, liliwatia hofu kubwa na kuwakatisha tamaa kabisa kwamba hakuna ushindi katika vita ile. Wengi wa maaskari wa jeshi la Makka walivunjika moyo, usiku ule ule wengi waliamua kuondoka bila hata ya kuwaaga wenzao. Kwa njia hii vita hii haikuendelea.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Sheria za Mahakama ya Qadhi sio za Kiislam, Biblia ni jibu acheni kupotosha watu

Na Mwalimu Kais Ali wa Mkongotema, Madaba Songea

Kutoka toleo lililopita

Ndugu zangu wapendwa angalieni wenyewe jinsi hawa jamaa Biblia ni Jibu walivyokuwa mabingwa wa upotoshaji wa aya za Mwenyezi Mungu, lakini sisi Waislam hatushangai kwa hayo wanayoyafanya ndugu zetu Wakristo kwa sababu Mwenyezi Mungu Alishaeleza mapema katika Kurani Tukufu kuhusiana na tabia za hawa ndugu zetu alisema kwamba; "Na kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, tumewalaani na tumeifanya mioyo yao kuwa migumu. Huyabadilisha maneno toka mahali pao, na kusahau sehemu ya yale waliyokumbushwa. Na utaendelea kupata habari za hiyana yao, isipokuwa wachache miongoni mwao. Basi wasamehe na waache, hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao hisani" (5:14). Kwa mantiki hiyo kwa ndugu zetu Wakristo tabia ya kubadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu ni tabia yao hawa ndugu zetu Wakristo wamebadilisha maneno mengi yaliyomo katika Injili kwa mfano Injili iliyopigwa chapa mwaka 1945 waraka wa Yuda (1:14) imesema kwamba; "Na Enok, wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hawo, akisema, angalia, Bwana alikuja na elfu kumi za watakatifu wake" Ni dhahiri kuwa utabiri huo unahusu kufika kwa Bwana ambaye ni Mtukufu Mtume Muhammad (saw) pamoja na watakatifu (Masahaba) elfu kumi, utabiri huo ulitimia wakati Mtume (saw) alipoiteka Makka pamoja na masahaba wake elfu kumi. Sasa Mapadre walipoona maneno hayo ni hatari kwa ajili yao na dini yao, mwaka 1950 maneno hayo wakayabadili na sasa katika Injili ya sasa maneno elfu kumi ya watakatifu yanasomeka; "Na Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao akisema, angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake maelfu maelfu" (Injili ya Union version).

Pia katika Injili ya Mathayo iliyochapishwa mwaka 1945 kuwa maneno yanayosema kwamba; "Hamtaimaliza miji yote ya Israeli hata ajapo mwana wa Adam" (Mathayo 10:23) waandishi wa Injili wamebadilisha maneno ya Injili ya mwaka 1950 aya hiyo imeandikwa hivi; "Hamtaimaliza miji ya Israeli" Neno "yote" limeondolewa maneno yapo



Mwalimu Kais Ali

mengi yaliyoondolewa na kubadilishwa na Wainjilisti wa Kikristo lakini siwezi kuyaeleza yote kwa kuwa nafasi haitoshi na tunaambiwa ya kuwa Injili hizi zote zimeandikwa kwa mwongozo war oho mtakatifu na hata ile aya ya Injili inayoruhusu Wakristo kunywa pombe nayo pia tunaambiwa iliandikwa kwa mwongozo war oho mtakatifu soma maneno haya yanayopatikana katika kitabu cha (1 Timotheo); "Usinywe maji tu, bali unywe divai (pombe) kidogo kwa ajili ya tumbo lako, kwaani unaugua mara kwa mara" (5:23). Kwa hiyo imebakia kwa msomaji mwenyewe kutafakari na kuangalia juu ya hali hiyo inayopatikana katika Injili sisi Waislam tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetupatia mwongozo wa Kurani Tukufu kitabu kisichobadilika maneno yake kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe Alisema na kutoa ahadi kwamba atakilinda kitabu hiki cha Kurani Tukufu, Amesema Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu kwamba; " Hakika Sisi Tumeteremsha mawaidha na hakika Sisi ndio Tuyalindao" (15:10) ahadi hiyo ya Mwenyezi Mungu ni ya ajabu imetimia barabara hata wapinzani waadilifu wa dini tukufu ya Kiislam wanakubali jambo hili kuwa Kurani hii ya leo ni ile ile iliyoteremshwa kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) soma maelezo ya Sir William Muir – (Introduction to the life of Muhammad). Pia Professa Noldeke, mwanachuoni msomi mustashriki (Orientalist) na mwingine mkuu wa kijerumani anakubali pia jambo hili (ENC. Brit). Pia na Professa Nicholson anakubali jambo hili la kuhifadhiwa kwa maneno ya Kurani Tukufu soma (Literary History of the Arabs). Ahadi hiyo ya kuhifadhiwa kwa maneno ya Kurani Tukufu inatosha kuhakikisha kuwa kitabu hiki cha Kurani Tukufu kimetoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa mantiki hiyo ujumbe na mafundisho aliyokuja nayo Mtukufu Mtume Muhamamd (saw) ni ya kweli.

Taasisi ya Biblia ni jibu katika machapisho yao wameeleza kuwa kwa mujibu wa aya ya Kurani Tukufu sura ya 2:209 inayosema kuwa "Enyi mlioamini, ingieni nyote katika utii …" inawataka watu wote hata wasiokuwa Waislam wafuate hukumu za Kiislam. Ndugu zangu wasomaji wapendwa maelezo hayo sio ya kweli, sheria za Kiislam zinawahusu wale tu, waliokubali kuwa wafuasi wa dini tukufu ya Kiislam hata ukiangalia aya hiyo hapo juu utaona ya kwamba wanaoambiwa hapo ni Wafuasi wa dini ya Kiislam kwa sababu aya imeanza na maneno "Enyi mliamini" yaani Enyi Waislam, kwa hiyo waaminio ndio Waislam walioamini Mungu ni mmoja na wala sio watatu na wakaamini Mtume Muhammad (saw) ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Kama aya hiyo hapo juu ingeanza kwa kusema kwamba Enyi watu ingeleta maana ya kuwahusu watu wote kwa hiyo sio kweli kusema kwamba sheria za Kiislam zinawahusu watu wote. Dini tukufu ya Kiislam Mwenyezi Mungu Ametoa tangazo la uhuru wa kuabudu kwa kila mtu kwa mfano katika Kurani Tukufu Amesema kwamba; "Hakuna karaha (kulazimishana) katika dini, hakika uongofu umekwisha pambanuka katika upotevu, basi anayemkataa shetani na kumwamini Mwenyezi Mungu, bila shaka yeye ameshika kishikio kigumu kisichovunjika, na Mwenyezi Mungu ni Asikiaye Ajuaye" (2:25) tena Mwenyezi Mungu Anasema "Na useme; kweli hii imetoka kwa Mola wenu, basi anayependa aikubali, na anayependa basi akatae …." (18:30) tena Mwenyezi Mungu Anasema; "Sema Enyi watu; hakika haki imekwisha wafikieni kutoka kwa Mola wenu, basi anayeongoka, anaongoka kwa faida ya nafsi yake, na anayepotea, basi anapotea kwa hasara ya nafsi yake, na mimi si Mlinzi juu yenu" (10:109) aya hizi zote hapo juu zinaonyesha kwa uwazi kuwa dini tukufu ya Kiislam haimlazimishi mtu kuingia katika dini ya Kiislam na wala mtu asiekuwa Mwislam halazimishwi kufuata sheria za dini tukufu ya Kiislam kwa nguvu bali mtu anatakiwa afanye uchunguzi na utafiti wa kina ili aupate ukweli wa dini ipi ni ya kweli.

Pia Biblia ni Jibu katika machapisho yao wamezungumzia habari ya mirathi katika dini ya Kiislam wamesema kwamba "Ikiwa ndugu yako aliyefariki ni Mwislam na wewe ni Mkristo wewe ambaye nni Mkristo huna haki ya kurithi mali yake". Pia wakasema "Mtoto wan je ya ndoa hana urithi kwa baba yake"

Majibu ya maelezo ya hapo juu kwa ndugu zetu Biblia ni Jibu ni kama ifuatavyo, hakupatikani mahala popote katika Kurani Tukufu ambacho ndicho kitabu cha sheria kwa Waislam, bali tunaona Mwenyezi Mungu Ametoa haki kwa ndugu wa marehemu bila kujali dini ya mtu ili muradi tu marehemu ni ndugu hivyo ndugu wa marehemu wana haki ya kumrithi ndugu yao aliyefariki, Mwenyezi Mungu Amesema katika Kurani Tukufu kwamba, "…….. na ngugu wa tumbo wana haki zaidi wao kwa wao katika kitabu cha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu" (8:76). Ama kuhusiana na mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa naye pia amepewea haki ya kumrithi baba yake endapo kama amefariki. Ifahamike kuwa anayetakiwa kumrithi baba ambaye ni marehemu ni mtoto wake wa kuzaa yeye mwenyewe marehemu kwa hiyo tunatakiwa tujuwe mtoto anapatikanaje kwa mujibu wa mafundisho ya Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Anasema kwamba; " …….(Ni haramu kuwaoa) wanawake wa wana wenu waliotoka katika migongo yenu, …." (4:24) tena Mwenyezi Mungu Anasema kwamba; "Basi mtu ajitazame ameumbwa kwa kitu gani, Ameumbwa kwa maji (manii) yaendayo kasi, yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo na mbavu" (86: 6 – 8) kwa mantiki hiyo endapo kama mume na mke wameshirikiana tendo la ndoa au kujamiiana iwe ndani ya ndoa au nje ya ndoa (zinaa) kitakachotokea baada ya kitendo hicho ni kuzaliwa mtoto, kwa hiyo ni dhulma kubwa sana kumnyima mtoto urithi wake kwa kosa walilolifanya wazazi wake kwani huyo mtoto hakuwatuma hao wazazi wake wamzae yeye mtoto huyo nje ya ndoa. Kama ni kuhukumiwa basi wazazi wa mtoto waliozaa nje ya ndoa ndio wanapaswa kuhukumiwa kama ni Waislam walitakiwa wacharazwe mijeledi (viboko) 100 tena bila kuhurumiwa, lakini kwa mtoto hana kosa lolote.

Biblia ni jibu tena wametoa lawama kuhusiana na sheria ya Kiislam ya kukata mwizi mkono. Ifahamike kuwa adhabu hii imekusudiwa kuung'oa kabisa wizi. Upo usemi unaosema kwamba ukicheka na nyani mwisho utavuna mabua hivyo basi ni bora mwizi mmoja akatwe mkono kuliko kumpa adhabu ya huruma na kuwafanya watu wengi kuwa wezi, hata hivyo hivi sasa baadhi ya wananchi wamejitungia sheria yao mwizi akikamatwa wanamchoma moto jambo ambalo ni kitendo kibaya sana kuliko kukata mkono na sheria hizi za kukata mwizi mkono au kuchapwa bakora wazinifu zitatumika katika nchi zile tu zinazojiita zinafuata sheria za Kiislam, lakini katika nchi zisizo kuwa za Kiislam hakuna ruhusa ya kutumia sheria hizo za Kiislam. Pia Biblia ni Jibu wamelaumu tena wakisema kwamba eti zipo sheria za Kiislam zinazoruhusu mzinifu mwanaume na mzinifu mwanamke wapigwe mawe mpaka kufa.

Ndugu wasomaji wapendwa sheria hiyo haipo katika Kurani Tukufu bali Mayahudi ndio walikuwa wanaitumia sawa na sheria ya Torati soma maelezo yafuatayo kutoka kwenye Biblia; "Mwanamume akimkukta msichana aliyechumbiwa, akalala naye, mtawatoa wote wawili nje ya mji na kuwapiga mawe mpaka wafe. Msichana huyo lazima auawe kwa kuwa hakupiga kelele asaidiwe ingawa alikuwa mjini, naye mwanamume lazima auawe kwa kuwa amemchafua mchumba wa jirani yake. Ndivyo mtakavyokomesha uovu huo miongoni mwenu". (Kumbukumbu ya sheria ya Torati 22:23 – 24). Tena Biblia inasema "lakini kama mashtaka hayoni ya kweli, na hakuna ushahidi wa ubikira wake, watampeleka kwenye mlango wa nyumba ya baba yake na wanamume wa mji huo watampiga mawe afe kwa sababu amefanya ufedhuli katika Israel kwa kufanya umalaya akiwa nyumbani kwa baba yake ndivyo mtakavyokomesha uovu huo miongoni mwenu". (Kumbukumbu la Torati 22:20 -21). Kumbe tumeshaona kuwa sheria hiyo ya kupiga mawe wazinifu walikuwa wanaitumia Waisraeli yaani Mayahudi na wala sheria hiyo haiwahusu Waislam. Bw. Yesu alisema kwamba; "Msiwahukumu wengine, nanyi hamtahukumiwa, msiwalaumu wengine nanyi hamtalaumiwa …. Luka 6:37. Tena Bw. Yesu alisema kwamba kwa nini wakiona kibanzi

Endelea uk. 10

Sheria za Mahakama ya Qadhi sio za Kiislam,

Kutoka uk. 9

jichoni mwa ndugu yako, na papo hapo huioni boriti iliyoko jichoni mwako? Au wawezaje kumwambia ndugu yako, ndugu ngoja nikuondoe kibanzi jichoni mwako, na huku huioni boriti iliyoko katika jicho lako mwenyewe? Mnafiki wewe, toa kwanza boriti iliyoko jichoni mwako, na hapo ndipo utaona sawa sawa kiasi cha kuweza kuondoa kibanzi kilicho jichoni mwa ndugu yako (Luka 6:41 – 42).

Kwa mantiki hiyo sawa na maelezo hayo ya Bw. Yesu hapo juu taasisi ya Biblia ni Jibu kwanza walitakiwa wasome maelezo ya kitabu chao cha Biblia kunakopatikana na sheria ya adhabu ya kupiga mawe wazinifu mpaka kufa ndipo angelinganisha na maelezo ya Kurani Tukufu kunakopatikana na sheria ya adhabu ya kucharaza bakora 100 wazinifu (Kurani Tukufu 24:3)

Kwa hiyo basi ndugu zangu Biblia ni Jibu inabidi wawaeleze watu ukweli kuwa sheria ya ahdabu ya kupiga mawe mzinifu mpaka kufa sio ya Kiislam bali sheria ya wale wanaofuata maneno ya Biblia ambao ni Wakristo na hata kama ikaonekana hivi sasa kwa baadhi ya nchi zinazojiita za Kiislam wanaitumia sheria hiyo ya kupiga mawe mzinifu mpaka kufa, isifahamike kuwa nchi hizo zinafuata sheria za Kiislam bali wao kwa hakika wanafuata sheria za mayahudi kwa sababu sheria za Kiislam ni zile zinazopatikana katika Kurani Tukufu kitabu ambacho ni maneno ya Mwenyezi Mungu.

Kwa mantiki hiyo na kwa maelezo hayo sasa imeshabainika kuwa kumbe sheria za Kikatili za kupiga mawe mzinifu sio za Kiislam, bali sheria hiyo inapatikana katika Biblia Takatifu.

Pia kuhusiana na amri ya kufunga saumu mwezi mtukufu wa Ramadhani sheria hiyo pia inawahusu Waislam tu, na wala haiwahusu watu wa dini zingine, na aya inayoelezea kuhusiana na amri ya kufunga saumu inaeleza wazi wazi kuwa atakayekuwa mgonjwa au yupo safarini basi asifunge saumu, kwa hiyo watu wa aina hiyo wagonjwa na wasafiri wanatakiwa wapate huduma za kibinadamu kula na kunywa kama kawaida katika mwezi huo wa Ramadhani. Kwa hiyo ni makosa makubwa sana kutangaza katika jamii kuwa katika mwezi mtukufu wa Ramadhani huduma za kibinadamu kama mahoteli au mikahawa ifungwe hakuna andiko lolote la Mwenyezi Mungu au la Mtume (saw) linalosema hivyo bali hayo ni maneno tu ya watu wa mtaani wasiojua vizuri mafundisho ya dini tukufu ya Kiislam. Pia Biblia ni jibu katika machapisho yao wametoa shutuma na lawama kubwa sana kuhusiana na sheria za Kiislam kuhusiana na adhabu ya mtu anayeritadi dini yaani anayeacha dini tukufu ya Kiislam. Ndugu hao Biblia ni JIbu wamenukuu Hadithi mbalimbali za uwongo walizosema eti Hadithi hizo ni za Mtume Muhammad (saw) kwamfano wamenukuu Hadithi hii; "Imesimuliwa na Abdullah Ibni Masud (ra) amesema si halali kumwaga damu ya Muislam anayekiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi kuwa hakuna Mola anayestahili kuabudiwa ispokuwa Allah na Mimi ni Mtume wa Allah sipokuwa kwa moja ya matatu haya, itauliwa nafsi kwa sababu ya kuua nafsi. Twayyib mzinifu aliyetoka katika dini mwenye kuacha kundi la Uislamu". (Sahihi Bukhari Vol.9. Hadithi No.17)

Tena wamenukuu Hadithi ifuatayo, "Mwenye kubadili dini yake muuwe" (Kitabu Min hajil Muslim Juzuu 3, Uk.300) Ndugu wasomaji wapendwa kama nilivyosema hapo mwanzoni mwa makala yangu kuwa Hadithi yeyote itakayokuwa kinyume na maneno ya Kurani Tukufu Hadithi hiyo ni ya uongo. Na ndivyo ilivyo kwa hadithi hizo zote hapo juu ni za uongo hazikusimuliwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwa sababu Hadithi hizo zinapingana na maelezo ya Kurani Tukufu. Mwenyezi Mungu Anasema katika Kurani Tukufu kwamba, wala hawataacha kupigana nanyi mpaka wawatoweni katika dini yenu kama wakiweza; na miongoni katika dini yake, kisha akafa hali yu kafiri basi hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika katika dunia na akhera, nao ndio watu wa motoni, humo watakaa (2:218) tena Mwenyezi Mungu Anasema; "Kwa hakika wale warudiao kwa migongo yao baada ya kuwabainikia mwongozo, shetani amewadanganya na kuwachelewesha" (49:26).

Tena Mwenyezi Mungu Anasema "Hakika wale walioamini, kisha wakakufuru, kisha wakaamini, kisha wakakufuru, tena wamezidi katika kufuru, Mwenyezi Mungu Hatawasamehe wala Hatawaongoza njia" (4:138).

Aya hizo zote hapo juu zinaeleza kwa uwazi sana kuwa mtu anayeacha dini ya Kiislam hakuna sheria ya kuuawa, bali mtu anaruhusiwa kuingia katika dini ya Kiislam akiamua anaweza kuacha hakuna sheria yeyote inayomkabili bali Mwenyezi Mungu Mwenyewe ndiye Atakayemhukumu. Baadhi ya Masheikh wanasisitiza adhabu hiyo ya kuritadi, ifahamike kuwa Masheikh hao wanafanya makosa makubwa sana kwa sababu Kurani Tukufu haiwaungi mkono hayo mawazo yao potofu. Dini tukufu ya Kiislam inatoa uhuru wa kuabudu. Na hata zama za Mtukufu Mtume Muhammad (saw) wapo watu ambao waliacha dini tukufu ya Kiislam lakini hawakufanyiwa kitu chochote.

Pia Biblia ni Jibu katika machapisho yao wameeleza kuwa sheria ya dini ya Kiislam inaruhusu kuwa wanaopinga maneno ya Kurani Tukufu na anayepinga sifa za mwenyezi Mungu au anayeonyesha dharau kwa Mwenyezi Mungu auawe wamenukuu aya ya Kurani Tukufu, kwamba; "Na kama ukiwauliza, lazima watasema; Sisi tulikuwa tukidhihaki na kucheza tu. Sema Je mlikuwa mkimfanyia mzaha Mwenyezi Mungu na aya zake na Mtume wake, msitoe udhuru, hakika mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu, kama tukilisamehe kundi miongoni mwenu tutaliadhibu kundi jingine kwa sababu wao walikuwa wakosefu" (9:65 – 66).

Ndugu wasomaji wapendwa aya hizo hapo juu zinazungumzia habari ya wanafiki hasa hasa zama zile za Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na ukiangalia aya zote zinazopatikana katika Sura Atauba zinaelezea amri ya jihad na habari za wanafiki waliokuwapo zama za Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Kwa mantiki hiyo sheria za dini ya Kiislam zinatoa haki na kulinda haki za kibinadamu. Na watu wa dini zingine wakitaka kuzijua sheria za za Kiislam basi wanatakiwa wasome maneno ya Kurani Tukufu ambayo ni ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na wala wasiangalie vitabu vingine vilivyoingizwa mikono ya watu au wasisome rain a maelezo ya Masheikh – wasiokuwa na elimu ya dini tukufu ya Kiislam, hivyo basi wakati tunaelekea kwenye mchakato wa kupata katiba mpya ningeishauri serikali kwamba kwa kuwa katiba yetu ya hivi sasa iliyotungwa mwaka 1977 toleo la mwaka 2005 ibara ya 19 – (2) inasema kwamba; "Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiyari la mtu binafsi, na shughuli na uendeshaji wa Jumuiyya za dini zitakuwa nje na shughuli za mamlaka ya nchi".

Ingekuwa ni kwa serekali kuzingatia kipengere hicho kwamba shughuli zote zinazohusu dini waachiwe wanadini wenyewe na taasisi zao kwa sababu serekali yetu sio ya dini Fulani, kwa sababu leo Waislam watadai serekali itambue mahakama ya Kadhi siku nyingine na Wakristo nao watadai kiingizwe kipengere chao kwenye katiba kwa hiyo matokeo yake kutakuwa na vurugu mechi ya sintofahamu. Namalizia kwa maneno ya Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ambaye ni Nabii aliyetumwa katika zama hizi na Mwenyezi Mungu ili kuja kuondoa matatizo kwa watu na kuwasuluhisha watu yeye alisema kwamba, "Ukweli ni ule ulioletwa na dini ya Kiislam na Mwenyezi Mungu Amenituma ili nioneshe nuru ile inayopatikana katika dini ya Kiislam,kwa wale wapendao kupata haki. Mwenyezi Mungu Amenituma ili nidhihirishe ukweli wa dini ya Kiislam katika dunia kwa ishara na msaada ulio ni roho hasa ya dini ya Kiislam. Mwenye bahati njema ni yule anayekuja kwangu kwa moyo laini kwa kupata haki, tena ni mwenye bahati njema yule ambaye anaiona haki na kuikubali".

Kwa mantiki hiyo hivi sasa watu wakitaka kuona ukweli wa mafundisho safi ya dini tukufu ya Kiislam wanakaribishwa katika Jumuiyya hii tukufu ya Waislam wa Ahmadiyya ambayo inayo mafundisho safi ya dini tukufu ya Kiislam, kwani ndio Jumuiyya pekee ya Kiislam duniani kote yenye mafundisho safi ya Kiislam yenye kuleta amani.

Maelewano katika jamii ya dini mbalimbali na makabila mbalimbali duniani. Mwisho nawaombea Mwenyezi Mungu Awaongoze watu wote wenye kutafuta haki na ukweli. (Amin).

= Mwisho=

TANGAZO LA IJITIMAA YA LAJNA NA NASIRAT 2014

Kwa Lajna na Nasiratul Ahmadiyya wote Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania.

Sadr Lajna Imaillah Tanzania anawatangazia wana Tanzeem wote kuwa, Ijtimaa yao kwa mwaka huu 2014 itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam kuanzia tarehe 27 hadi 29 mwezi wa Juni 2014.

Lajna na Nasirat wote nchini wanaombwa kujiandaa kushiriki pamoja na kutilia mkazo maelekezo yaliyomo katika barua za Ijtimaa zilizotumwa matawini. Aidha mkazo maalum uwekwe juu ya mashindano ya kielimu.

Pia wanakumbushwa kuhusu michango, kila mtu ahakikishe anamaliza michango ya Ijitimai hiyo. Yeyote atakayesoma tangazo hili amwambie na mwenzake.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Ajaalie mafanikio mema. Amin.

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Kutoka uk. 12

ilikuwa pale pale, lengo lake kwa sasa lilikuwa ni kwenda Afrika ya Kusini ili apate elimu. Enzi hizo kiwango cha elimu Afrika ya Kusini kilikuwa juu. Rafiki yake mmoja Mjini Dar es salaam alimueleza ya kwamba kulikuwa na uwezekano wa kupata kazi katika meli iliyoitwa; '……. *By Castle*'. Kwa njia hii angeliweza kuuwa ndege wawili kwa jiwe moja. Angelipata chochote na hicho kingemsaidia katika harakati zake za kupata elimu.

Hivyo akaacha kazi katika shirika la reli la Afrika Mashariki. Safari yake ilianzia Tabora na kufika Dar es salaam. Maisha ya Dar es salaam yalimpa picha ya mateso yaliyokuwa yanaendelea nchi nzima. Ubaguzi, unyanyasaji, dharau n.k Katika kipindi hicho akaandika barua ya maombi ya kazi. Jibu alilopata liliweka msumari wa moto kwenye donda. Walimueleza kwamba meli ilikuwa haiajiri watu weusi. Lilikuwa ni tusi kubwa. Mtu hakupimwa kwa uwezo wake bali kwa rangi yake. Jambo hili lilimuongezea tashwishi ya kuendeleza mapambano dhidi ya dhuluma. Katika hali hiyo hakujua jambo la kufanya. Alikuwa amepoteza kazi na hakufaninkiwa kupata kazi. Mwaka 1930 hakuwa na njia nyingine isipokuwa kurudi katika shirika la reli la Afrika Mashariki. Muda si mrefu alikuwa msaidizi mkuu wa kituo (Station Master) kwa miaka miwili alifanya kazi na mwaka 1932 alijiuzuru tena shirika la reli. Mwaka 1933 alipata kazi idara ya mipango Dodoma.

Mchango wa Hassan Suleiman Toufiq katika harakati za kueneza habari za uhuru zinajitokeza zaidi 1933 aliposhiriki katika kuanzisha tawi la kwanza la *Tanganyika African Association* nje ya Dar es salaam. Tawi hilo lilianzishwa Dodoma tarehe 26/04/1933. Umuhimu wa tawi hili ni kwamba lilikuwa la kwanza kuanzishwa nje ya Makao Makuu ya TAA yaani Dar es salaam na hivyo kutoa changamoto kubwa ya kueneza TAA nchini. Hassan Suleimani Toufiq amepewa lakabu ya *Yohana Mbatizaji* ambaye alipita nchi nzima akifungua matawi na kueneza ujumbe wa kupigania haki za wanyonge. Hassan Suleiman Toufiq ndiye aliyemtoa mwari ndani. Toka 1941 hadi 1945 alitembelea nchi nzima akifungua matawi na kuifikisha TAA kwa watu. Kabla ya hapo ilikuwa ni mali ya watu wa Dar es salaam na wasomi wachache. Aliyafumbua macho ya watu kwamba kuna mkombozi wa wanyonge ni Hassan Suleiman Toufiq.



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa kwenye tafrija ya kusherehekea uhuru wa Tanganyika na Dar es Salama kupewa hadhi ya jiji - Sheikh Kaluta Amri Abedi akiwa Meya wa kwanza Mwafrika wa Jiji hilo.

Mwaka 1945 Hassan Suleiman Toufiq alipita Tabora katika harakati zake za kueneza ujumbe wa uhuru na hapo alifungua tawi la TAA na kumpata mwanachama ambaye baadae alikuja kukitumikia chama cha TANU na mwanachama huyo ni Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa anafundisha shule ya Mtakatifu Mary Tabora. Nyerere alijiunga na TAA na kuchaguliwa kuwa Katibu msaidizi wa TAA. Kazi ya kumwingiza Nyerere katika TAA ilikuwa ni ya Hassan Suleiman Toufiq.

Kama tulivyokwisha sema TAA Makao Makuu ilikuwa imesinzia. Ni tawi la Dodoma likiongozwa na Hassan Suleiman Toufiq lililokuwa moto moto na kufunika kabisa Makao Makuu. Tawi hilo lilipita huku na kule na ndio lilianzisha uhusiano na Zanzibar, jambo ambalo hatimaye vikaingia vyama vya TANU / Afro-Shiraz na hatimaye muungano. Unawezaje kuzungumzia muungano wa Tanganyika na Zanzibar bila kumtaja Hassan Suleiman Toufiq?

Tawi la Zanzibar ambalo ni matunda ya Hassan Suleiman Toufiq lililoitisha mkutano wa kwanza wa kitaifa wa TAA na hili liliudhi sana Makao Makuu. Ili kumaliza kutoelewana uliitishwa mkutano Dar es salaam mwaka 1944 mwezi wa Septemba. Tawi la Dodoma lilimtuma Hassan Suleiman Toufiq na vikao vine vilifanyika toka tarehe 15 hadi 18 Septemba 1944. Katibu wa Dar es salaam P. Mmtambo alifungua mkutano kwa kumuliza kwa nini walikuwa wameomba mkutano. Bwana Hassan Suleiman Toufiq mwanasiasa aliyetawaliwa na kusema kweli bila ya woga wowote, alisema ya kwamba wangelipenda kujua kwa nini Dar es salaam (Makao Makuu) tawi lilikuwa limezorota na kuonesha dalili za kurudi nyuma. Mjumbe mwingine Salim Juma alitaka kujua kwa nini Makao Makuu yalikuwa hayajibu barua kutoka matawi mengine. Maswali hayo yalijibu lakini ikaonesha ulikuwepo upungufu.

Hassan Suleiman alikieleza kikao hicho dhamira yake ya kufungua matawi zaidi nchini. Alishauri pia ufanyike mkutano mwingine wa kitaifa mwaka 1945. Jambo ambalo alishauri Hassan Suleiman Toufiq lilikuwa ni ombi la kukutana na viongozi wengine wa vyama vingine vya Waafrika. Aliweza kukutana na viongozi wa *African Government Employees Association, Tanganyika Railway African Employees Association, Teachers Association*. Hawa wote aliwauliza kwa nini walikuwa hawaiungi mkono TAA na aliwahakikishia ya kuwa TAA haikuwa na ugomvi na serikali. Kwa mara ya kwanza Hassan Suleiman Toufiq alifungua mlango wa ushirikiano baina ya chama cha siasa na vyama vya wafanyakazi. Na hii ndio sera aliyoitumia Julius Kambarage Nyerere wakati aliposhirikisha vyama vya wafanyakazi chini ya Rashidi Mfaume Kawawa katika harakati za kudai uhuru.

Katika kuzunguka kwake alikemea kwa nguvu zake zote ukabila na uhasama wa dini. Katika mikutano aliyohutubia alieleza faida za umoja na ushirikiano usiojali dini wala cheo cha mtu. Licha ya kukieneza chama cha TAA nchini alifungua milango pia ya kuwa na uhusiano na Pan – Africanism ya akina George Padmore waliopigania uhuru, heshima na ukombozi wa mtu mweusi. Mbegu ya sera za kuenzi utu wetu waafrika, kupigania uhuru na kuleta muungano wa nchi za Kiafrika ni fikra pevu ambazo Hassan Suleiman Toufiq alizichota kwa mwanamajmui (*Pan africanist*) aliyebobea George Padmore. Na kukamilisha mchango wa Hassan Suleiman Toufiq wa ukombozi wa nchi ni pale mwaka 1953, Hassan Suleiman Toufiq alipomtambulisha Oscar Kambona kwa Mwalimu Nyerere. Kambona alikuwa mwalimu shule ya Dodoma Alliance na mchango wake kwa ukombozi wan chi hii ni wakuheshimiwa sana. Alikuwa Katibu Mkuu wa TANU, waziri wa elimu, Waziri wa mambo ya ndani, Waziri wa mambo ya nchi za nje na Waziri wa Maendeleo ya Mikoa. Mchango wake katika ukombozi ni mkubwa na wa kuheshimiwa.

Kwao neno zima fikra za baadae za Mwalimu Nyerere kuhusu siasa za nchi inaonesha alijifunza kutoka kwa Hassan Toufiq. Wazo la kupeleka TAA kwa watu na sio ibaki tu mjini ni wazo la Hassan Suleiman Toufiq. Kwa vitendo Mwalimu Nyerere alikuja kupeleka TANU kwa watu vijijini. Mbegu ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar ilipandwa na Hassan Suleiman Toufiq alipopeleka TAA hadi Unguja. Na moja ya sifa ya Mwalimu ni kusaidia katika kuleta muungano baina ya Tanganyika na Unguja. Kwenye mikutano ya hadharaHassan Toufiq alikemea ukabila na mambo ya dini akililia umoja na mshikamano. Akizungumzia miaka mingi baadae dhana ya nyufa zilizoingia katika taifa letu. Mwalimu Nyerere bila shaka alikuwa anapita mle mle alimopita Hassan Suleiman Toufiq miaka mingi iliyopita. Uanamajmui, umoja wa watu weusi, kupigania ukombozi na shirikisho la bara la Afrika ilikuwa njozi kubwa ya Hassan Toufiq Suleiman. Wachunguzi wa mambo ya siasa wanaheshimu sana mchango wa Julius Nyerere katika ukombozi na kuleta umoja wa Afrika. Hatuwezi kudharau aliyojifunza kutoka kwa Hassan Suleiman Toufiq. Hatuwezi kuelewa hatima ya nchi hii ingekuwaje bila ya wanasiasa wa makamu ya Hassan Suleiman Toufiq aliyekuwa na uwezo wa kutizama katika mbegu ya wakati na kutuonesha mbegu itakayo ota na kuchipua. Mpandaji alipanda mahali penye mboji na mmea wa uhuru ukamea. Mpandaji wa mbegu hiyo ni Hassan Suleiman Toufiq na ardhi yenye mboji na rutuba ni Julius Kambarage Nyerere. Ni muungano wa sifa mbili hizi ndio maana tuna taifa tulilonalo kwa hivi sasa.

=Itaendelea toleo lijalo=

Aongoza somo la Hisabati

Kutoka uk. 12

kumbukumbu za dunia kwa ugunduzi na umahiri mkubwa katika fani ya somo la fizikia hapa duniani.

Hapa Afrika tunayo majina ya kutaja katika namna ya pekee, wanafunzi waliopita shule ya Tabora kama Marehemu Jumanne Abdallah, Mzee Bakari Rashid Kazema, Sheikh Kaluta Amri Abeid na wengineo wanakumbukwa kwa jinsi walivyokuwa mahiri katika masomo na walivyojitolea katika kuitumikia Islam. Hivi karibuni Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania imetoa tafsiri mpya ya Qur'an Tukufu katika lugha ya kiyao aliyotafsiri Mzee Alli Said Mosse. Hii ni kazi nzuri na ya kwanza kufanywa na muislam wa kwanza hapa nchini mwenye shahada ya uzamili ya uchumi aliyosoma nchini Uingereza kutafsiri Qur'an katika lugha hiyo kubwa nchini Malawi.

Ni vyema wasomi wengine wa kiislamu wakaiga mwenendo huu badala ya kutumia muda mwingi kuitafuta dunia ambayo maisha yetu hapa ni mafupi sana.

Safari ya Fuad Ahmad Khawaja ni ndefu na tunamuomba Mwenyezi Mungu azitumie hesabu zake kwenye kuitumikia Jumuiya na amfikishe kwenye kilele cha mafanikio kwa hapa duniani na kesho akhera. Amin.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Rabiul II/Jamad I 1435 AH | March 2014 | Amman 1393 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Amr bin Aasya kwamba mtu mmoja alimwuliza Mjumbe wa Allah s.a.w. kwamba Islam gani ndiyo bora? Akasema: Kulisha chakula na kumtolea salam kila unayemjua na usiyemjua (*Bukhari*)

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Na Mahmood Hamsin Mubiru - Dar es salaam

Kutoka Toleo lililopita

Dr. Kwegyia Aggrey aliwahi kutembelea baadhi ya shule na moja ya shule alizozitembelea ni ile ya Kilosa alikokuwa akisoma Hassan Toufiq Selemani mahiri wa hisabati katika darasa lake. Siku alipofika dr. Aggrey pale shuleni mwalimu wa darasa akauliza swali, ikiwa mtu alikuwa na shilingi saba na akanunua kuku watatu na bata, kuku mmoja shilingi mbili, bata alinunuliwa kwa bei gani? Aliyetoa jibu na kumfurahisha Dr. Aggrey ni Suleiman Toufiq ambaye anayo sifa ya kueneza ujumbe wa uhuru Tanzania nzima. Ushuhuda huu unatolewa na Mohamed Saidi katika kitabu chake; "*The Times and life of Abdulwahid Sykes*" anaposema *Hassan Suleiman mpanga mipango mahiri wa mambo ya siasa kati ya vita kuu mbili za dunia.*

Hassan Toufiq Sulaiman mwana wa Toufiq Suleiman alizaliwa tarehe 05 Septemba 1912 katika kijiji cha Msanga maili 23 mashariki ya mji wa Dodoma.



Sir Muhammad Zafrullah Khan (anayepunga mkono) alipowasili katika uwanja wa ndege wa Dar es Salaam alipotembelea hapa nchini mara baada ya uhuru wa Tanganyika kwa mwaliko rasmi wa Mwalimu Nyerere.
Sir Muhammad ambaye alikuwa ni Sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa a.s., Hakimu wa Mahakama kuu ya dunia na Mwenyekiti wa Umoja Umoja Mataifa mwaka 1962 alikuwa ndiye wakili wa Mwalimu Nyerere katika kudai uhuru wa Tanganyika kule Umoja wa Mataifa.

Baada ya masomo yake alijiriwa na shirika la reli kama mtuma simu. Mwaka 1926 alipelekwa masomoni Dar es salaam. Huko alikutana na vuguvugu na wanaharakati waliokuwa wanalalamikia uonevu waliokuwa wanafanyiwa watu weusi. Gumzo juu ya dr. Aggrey kutoruhusiwa kulala hoteli ya New African Hotel lilikuwa bado linaendelea. Akiwa Dar alijifunza mengi na kuona mengi. Alipomaliza masomo yake alipelekwa Malagarasi. Hapo alikorofishana na Muhindi kwani hakukubali kuonewa. Mwaka 1927 alihamishiwa Itigi. Rohoni aliendelea kusononeka kutokana na dharau waliyokuwa wanafanyiwa watu weusi. Siku moja Mzungu alimnasa kibao kwa kosa la kumsalimu katika Kiingereza! Hali hii iliweza kumsumbua na akaona njia ya kujikomboa ni kupata elimu. Akaanza bidii ya kusoma na katika usomaji wake ndipo alipokutana na maandishi ya Jumuiyya na miaka ya 1930 akajiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Dhamira yake ya kupata elimu

Endelea uk. 11

Ahmadiyya aongoza somo la Hisabati Afrika Mashariki.

Na Pazi Mazongera

Ile bishara aliyopewa Masihi Aliyaehidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) kuwa wafuasi wake watakuwa watakuwa wanang'aa katika mambo mbalimbali imetimia kwa hapa Afrika Mashariki. Kijana anaesoma shule ya Jaffery Academy mjumbe wa Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya aitwae Fuad Ahmad Khawaja kutoka Jamaat ya Arusha nchini Tanzania amefanikiwa kuwa mtu wa kwanza katika somo la hesabu katika ukanda wa huu wa Afrika Mashariki.

Habari zilizotufikia chumba chetu cha habari ni kwamba, kijana huyo amekuwa nguli wa hesabu kufuatia kuongoza katika somo hilo kwa muda mrefu na kufanikiwa kuwa wa kwanza na kutunukiwa heshima hiyo na baraza la mitihani lililofanyika tarehe



Fuad Ahmad Khawaja - bingwa wa hisabati Afrika Mashariki

27 Januari mwaka huu mjini Nairobi nchini Kenya.

Wakati tunafurahia matokeo mazuri ya kijana huyu, tunapaswa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuwafanya wafuasi wa Jumuiya hii kupata matokeo mazuri ya kimasomo darasani na katika Nyanja mbalimbali za kimaisha. Hii inathibitisha na kutimia kwa biashara ya Seydna Ahmad (as) juu ya wafuasi wake kupata mafanikio katika maeneo mbalimbali.

Tukio hili linatukumbusha juu ya wafuasi wa jumuiya hii ambao wamepata mafanikio makubwa ya kielimu na kimaisha na huku wakiwa ni watu wenye kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu na kujitolea zaidi. Anakumbukwa sana Muislam wa kwanza kupata heshima ya kuitwa *Sir*, muislam wa kwanza kuongoza Mahakama ya dunia 'the hague', mwanasheria mkubwa na waziri wa kwanza wa mambo ya nje nchini Pakistani baada ya kujitenga na India, huyu si mwingine bali ni Sir Muhammad Zafrullah Khan ambaye alikuwa ni sahaba wa Seyydna Ahmad (as). Wasifu wake ni mkubwa na kurasa chache za gazeti hili hazitoshi kuandika hata robo ya historia yake. Vitabu vingi ameandika, makala mengi yameeleza juu wasifu wa wacha Mungu wengine kikiwemo kitabu chake maarufu cha maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad (saw).

Tunamkumbuka pia Profesa Abdul Salaam, mwanafizikia wa kwanza Muislam kutunukiwa nishani ya amani ya nobel, muislam wa kwanza kupewa uraia wa heshima na Taifa la Italia kwa sababu ya taaluma yake. Ameingia kwenye

Endelea uk. 11